# Nipashe

Jumanne Agosti 18, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580313

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

…rdian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Kiama cha VICOBA, taasisi hewa za ukopeshaji fedha chaja rasmi

UKURASA 2




UKURASA 11

# Wagombea ubunge wa CCM mguu sawa

• **Watia** nia wote watakiwa kubaki majimboni, NEC yanoa panga, watakaopitishwa kujulikana Alhamisi... *Endelea ukurasa 2*


## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**MAITI YADAIWA KUZUIWA KISA KUTOLIPIA GHARAMA**

MWILI wa Herman Kamwela (65), mkazi wa Kijiji cha Isoko Wilaya ya Ileje mkoani Mbeya, umedaiwa kuzuiwa...

UKURASA WA 4

**WATUMISHI NARCO MATATANI TUHUMA UPOTEVU WA NG'OMBE**

MKUU wa Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, Onesmo Buselu, ameagiza Jeshi la Polisi kuwakamata watumishi...


## Ajali ya basi, lori yaua watu 4

UKURASA 3




Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) anayemaliza muda wake, Rais John Magufuli akikabidhi uenyekiti kwa Balozi wa Msumbiji nchini, Monica Patricio Clemente, ambaye alipokea kwa niaba ya Rais wa nchi hiyo, Filipe Jacinto Nyusi, katika Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store


# JPM akabidhi kijiti SADC ataja mafanikio manane

UKURASA 2


**MICHEZO** SIMBA, YANGA NANI ZAIDI OKT. 18 UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Kiama VICOBA mfukoni chawadia

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

SERIKALI imewataka watoa huduma ndogo za fedha kujisajili na kukata leseni kabla ya Oktoba 31, mwaka huu.

Muda huo ni wa mwisho kwa kipindi cha mpito kilichowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2019 kabla ya sheria hiyo kuanza kutumika rasmi Novemba Mosi, mwaka huu.

Agizo hilo lilitolewa jana mjini hapa na Kamishna wa Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha katika Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Charles Mwamwaja, kwa niaba ya Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Adolf Ndunguru wakati akifungua mpango wa utoaji elimu kwa umma kuhusu Sera, Sheria na Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha kwa wadau wa sekta hiyo, kutoka Kanda ya Kati inayojumuisha mikoa ya Dodoma, Singida na Iringa.

Dk. Mwamwaja alisema lengo la kusajili na kutoa leseni kwa watoa huduma hao ni kuiwezesha serikali kuwatambua ili kuboresha usimamizi na udhibiti wa sekta ndogo ya fedha nchini na kuwa na sekta ya fedha iliyo endelevu na yenye kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini.

"Sekta hii inatoa huduma za fedha kwa wananchi wa kipato cha chini ambazo zinachangia kuinua uchumi na kuongeza kipato. Kwa mujibu wa utafiti wa Finscope wa mwaka 2017, asilimia 55.3 ya nguvukazi ya taifa wanapata huduma za fedha kutoka taasisi za huduma ndogo za fedha," alisisitiza.

Alisema kutokana na umuhimu huo, serikali imekuwa ikitoa elimu ya kuwawezesha wananchi kutekeleza sheria hiyo na mpango wa utoaji elimu hiyo uliozinduliwa rasmi Desemba, mwaka jana na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango."Serikali itahakikisha elimu hii inaendelea kutolewa nchi nzima ili kuhakikisha wadau wote muhimu wanafikiwa na elimu hii na kuwawezesha kufuata matakwa yote ya kisheria kwa maendeleo ya uchumi wa nchi," alisema.

# Wagombea ubunge CCM sasa 'mguu sawa'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAGOMBEA ubunge kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), wanatarajia kujulikana wiki hii baada ya kupitishwa na Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya chama hicho kitakachofanyika kuanzia keshokutwa mjini hapa.

Kutokana na hatua hiyo, CCM imewataka watia wote wa ubunge wa majimbo na viti maalum kubaki katika maeneo yao ili baada ya majina ya wagombea waliopita kutangazwa waanze kuchukua fomu.

Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, alisema hayo jana jijini hapa baada ya kuzindua kituo cha mawasiliano ndani ya chama ambacho kinaunganisha mabalozi 2,500 nchi nzima na kitatumika kwa ajili ya kutoa na kupokea taarifa kutoka katika ngazi mbalimbali za chama.

Alisema vikao vya kuandaa nyaraka na kuchambua taarifa kutoka ngazi za wilaya na mikoa kuhusu wagombea wa ubunge majimboni na viti maalum vimeanza na kwamba Sekretarieti ya NEC ndiyo inafanya kazi hiyo.

Dk. Bashiru alisema baada ya uchambuzi, taarifa hizo zitafikishwa leo kwenye Kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (CC-NEC) kwa ajili ya mchakato wa uteuzi utakaofanyika keshokutwa. "Leo (jana) tunachambua mapendekezo ya vikao. Sekretarieti huwa haiteui, inaandaa nyaraka, kuchambua taarifa na kushauri vikao. Kesho (leo) tutafanya kikao cha Kamati Kuu na Agosti 20 (keshokutwa) tutafanya kikao cha Halmashauri Kuu na ndiyo tutajua majina ya walioteuliwa," alisema.

Kadhalika, Dk. Bashiru alisema Agosti 25, mwaka huu, wagombea watakaopitishwa na NEC watapaswa kuzifikisha fomu hizo Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa ajili ya uteuzi. "Tunatarajia kuwa sifa za chama chetu ndizo msingi mkubwa na uteuzi utazingatia mtu mchapa kazi, mzalendo, msikivu na mwenye nidhamu ya kutii vikao vya chama," alisema.

"Matarajio yangu kwa sababu tulikuwa na wagombea zaidi ya 10,000 naamini tutapata wagombea bora kwa sababu mchakato ulikuwa wa wazi," alisema Dk. Bashiru.

Kuhusu kituo cha mawasiliano na habari, Dk. Bashiru alisema zaidi ya mabalozi wa mashina 250,000 wameunganishwa kwenye kituo hicho kwa lengo la kuripoti habari za uchaguzi.

Alisema lengo la kuanzisha kituo hicho ni kuboresha mifumo ya utendaji katika chama.

"Tulikuwa hatuna mfumo wa kuwasiliana na umma na wanachama wakati tunataka kupokea au kutoa taarifa. Sekretarieti ilikaa na kuamua kuanzisha kituo hicho na kazi kubwa ya kituo ni kujenga daraja la mawasiliano kati ya umma, wanachama na uongozi wa makao makuu ya chama," alisema.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza wakati akifungua mkutano wa viongozi wa dini kuelekea uchaguzi mkuu na kuunga mkono juhudi za Rais John Magufuli na serikali yake katika ustawi wa amani, uzalendo na kumtanguliza Mungu, uliofanyika jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: OWM**

# JPM akabidhi kijiti SADC akitaja mafanikio manane

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS John Magufuli amekabidhi uenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa Msumbiji, huku akitaja mafanikio manane yaliyopatikana katika uongozi wake ikiwamo kuandaa Dira ya Maendeleo ya jumuiya hiyo ya mwaka 2050.

Akizungumza jana katika mkutano wa 40 wa Wakuu wa Nchi na Serikali za SADC uliofanyika kwa njia ya mtandao, Rais Magufuli alisema mbali na dira hiyo, pia wameandaa mpango elekezi wa maendeleo ya kikanda wa mwaka 2020-2030. "Kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita, tumesimamia uandaaji wa ajenda za SADC baada ya mwaka 2020. Kama mnavyofahamu, tangu mwaka 2000, ajenda za maendeleo ya jumuiya yetu zimekuwa zikisimamiwa mikakati mikuu miwili.

"Mipango hiyo ni ya mkakati elekezi wa maendeleo ya kikanda (RISDP) mwaka 2015 na mpango mkakati wa asasi ya siasa, ulinzi na usalama awamu ya pili. Mikakati yote inafikia ukomo mwishoni mwa mwaka 2020.

"Hivyo, katika kipindi cha uenyekiti wetu, tumeandaa dira ya maendeleo ya SADC ya mwaka 2050 pamoja na mpango elekezi wa maendeleo ya kikanda wa mwaka 2020 hadi 2030 na nyaraka hizi zitajadiliwa kwenye mkutano huu, zitatoa mwelekeo mpya wa kufikia malengo ya SADC tunayoitaka," alisema.

Rais Magufuli pia alisema kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, SADC chini ya uenyekiti wa Tanzania ilisimamia uandaaji wa miongozo kwa ajili ya kuimarisha na kuratibu ufanyaji biashara mipakani, akibainisha kuwa wananchi wameendelea kufanya biashara licha ya kuwapo kwa ugonjwa huo.

Pamoja na hilo, Rais Magufuli pia alisema kwa kipindi hicho wamesimamia ajenda ya SADC kuhusu maendeleo ya viwanda kwa kutumia kaulimbiu ya mkutano wa 39 ya 'Mazingira Wezeshi kwa Ajili ya Maendeleo Endelevu na Jumuishi ya Viwanda, Biashara na Ajira Ndani ya SADC'.

"Tulizihimiza nchi kuweka kipaumbele siyo tu katika ujenzi wa viwanda, lakini pia kutengeneza mazingira mazuri ya kustawisha maendeleo ya ukuaji wa sekta ya viwanda katika ukanda wetu. Moja ya kichocheo muhimu ni upatikanaji wa umeme wa uhakika," alisema.

Alibainisha kuwa kwa kipindi hicho cha mwaka mmoja, jumuiya imeongeza MW 3,595 kati ya MW 4,000 zilizotakiwa kuongezwa.

Aliyataja mafanikio mengine kuwa ni kuridhiwa kwa lugha ya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha nne za SADC, lugha hiyo sasa inatumika kwenye vikao vya wakuu wa nchi wanachama na hivyo kutachochea ushirikiano na utengamano kwa jumuiya.

Magufuli alisema nchi wanachama zitakuwa zikiadhimisha siku hiyo kwa kufanya mambo mbalimbali ikiwamo kuandaa makongamano, midahalo au kutoa matamko yenye kupinga vikwazo kwa Zimbabwe na mwaka jana ilitekelezwa azimio hilo.

"Mafanikio yameanza kupatikana. Mathalani, Umoja wa Ulaya umeanza kuona umuhimu wa kutatua mgogoro wa kibinadamu nchini humo kwa kutoa misaada na kusaidia utaalamu kwenye sekta mtambuka za maendeleo ya kiuchumi, huduma za msingi za afya na kujenga uwezo Zimbabwe kuhimili maafa na kufanikisha utoaji wa misaada mingine ya kibinadamu," alisema.

Kuhusu ulinzi na usalama, Rais Magufuli alisema katika kipindi hicho cha mwaka mmoja, wamejitahidi kusimamia jukumu hilo kikamilifu hususan kwa kuhakikisha amani na usalama unaendelea kutawala na kushughulikia migogoro kwenye nchi ya DRC na Lesotho.

Rais Magufuli alisema mafanikio mengine ni kusimamia masuala ya utengamano wa kiuchumi, akikumbusha kuwa mkutano wa 39 walizindua mfumo wa uombaji na utoaji vyeti vya utambuzi wa uasili wa bidhaa kwa njia ya mtandao ambao utarahisisha ufanyaji biashara mipakani.

# CUF yatangaza wagombea ubunge

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimetangaza majina ya wagombea ubunge katika majimbo 148 Tanzania Bara.

Aidha, majimbo manne kati ya 148 yatarudia kura za maoni kutokana na changamoto zilizojitokeza wakati wa kura za maoni.

Katika orodha hiyo ya wagombea ubunge, sura nyingi zilizochomoza ni mpya.

Miongoni mwa waliochomoza katika majina hayo ni pamoja na aliyewahi kuwa Mbunge wa Maswa Mashariki kupitia CHADEMA ambaye kwa sasa anagombea katika jimbo hilo hilo kupitia chama hicho (CUF), Sylvester Kasulumbayi.

Mwingine ni aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kaliua katika bunge la 11, Magdalena Sakaya ambaye ni Naibu Katibu Mkuu wa CUF, Tanzania Bara.

Wengine ni Abdul Kingwendu atakayepeperusha bendera ya chama hicho katika Jimbo la Ilala, Magdalena Dhangai (Arusha), Raphael Ngonde (Mbeya Mjini) na Fatuma Msuya (Moshi Mjini).

Sura nyingi mpya katika baadhi ya majimbo hayo ni pamoja na Abdul Kambaya (Mbagala), Sabrina Sungura (Segerea), Ngwale Kinjekitile (Mkuranga), Fatuma Pangalungome (Ukonga), Salama Masoud (Kigamboni) na Rajabu Salum (Kinondoni).

Pia wamo Salmini Kisamo (Kawe), Zainabu Amiri (Temeke), Mashaka Ngole (Ubungo), Hilda Mriya (Kibamba), Khalifa Mgonela (Kibaha Vijijini) na Chuma Salenge (Rufiji).

Kibiti ni Mohamed Ungaunga, Hadija Dikulumbale (Kisarawe), Mohamed Ngulangwa (Bagamoyo), Mwajuma Songoro (Kibaha Mjini), Abed Mlapakolo (Morogoro Mjini).

Wakati wagombea hao wakitangazwa, majimbo ambayo yatatakiwa kurudia uchaguzi wa kura za maoni ni Mbogwe, Arumeru Magharibi, Chalinze na Mwanga.

Mkurugenzi wa Mipango na Uchaguzi wa CUF Taifa, Juma Kilaghai, alisema uchaguzi katika majimbo hayo utarudiwa kutokana na sababu ambazo zilijitokeza wakati wa kura za maoni.

# Mwili wadaiwa kuzuiwa Mloganzila siku 5 kisa kukosa kulipa gharama

**Na Thobias Mwanakatwe**

MWILI wa Herman Kamwela (65), mkazi wa Kijiji cha Isoko Wilaya ya Ileje mkoani Mbeya, umedaiwa kuzuiwa kwa siku tano katika Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila kutokana na ndugu na jamaa zake kushindwa kulipa gharama za matibabu Sh. 1,581,426.

Ofisa Habari wa Hospitali ya Muhimbili- Mloganzila, Neema Mwangomo, akizungumza na Nipashe jana, alithibitisha Kamwela kufariki katika hospitali hiyo Agosti 12, mwaka huu na gharama alizokuwa akidaiwa.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Machimbo, Mariam Machicha, alisema mwananchi huyo ambaye hana ndugu jijini Dar es Salaam alifariki dunia Agosti 12 mwaka huu, ambapo hadi jana (Jumatatu) mwili wake uliendelea kuwa hospitalini.

Alisema Kamwela ambaye alikuwa akisumbuliwa na magonjwa mbalimbali, mara ya kwanza alipelekwa katika zahanati ya Segerea baadaye Hospitali ya Amana na Julai 26, mwaka huu alihamishiwa katika Hospitali ya Mloganzila ambapo alikuwa akipatiwa matibabu hadi mauti yanamkuta.

"Kamwela alikuwa mkazi wa mtaa wangu na hakuwa na ndugu yeyote hadi alipofariki wananchi wa mtaa huu nikiwamo mimi tulikwenda Mloganzila kwa lengo la kuchukua mwili ili tukazike, lakini tukaambiwa na uongozi wa hospitali hatuwezi kuuchukua hadi tulipe gharama za matibabu 1,581,426, tukashindwa," alisema Machicha.

Mwenyekiti huyo alisema baada ya kuelezwa hivyo walikwenda ofisi ya ustawi wa jamii ili kuomba msaada na baada ya kupewa kibali bado uongozi wa Hospitali ya Mloganzila uliendelea na msimamo kwamba kama hana ndugu wananchi wa mtaa huo wachangie ndipo wauchukue.

Machicha alisema baada ya kuelezwa hivyo, aliwaeleza wakazi wa mtaa huo ambao walisema hawana uwezo wa kulipia gharama za matibabu ila kama hospitali hiyo itawapa mwili wa marehemu watachangia fedha kwa ajili ya kukamilisha taratibu za maziko.

"Juzi Agosti 16 niliitisha mkutano wa wananchi kuwaeleza majibu niliyopewa Mloganzila wakasema hawawezi kuchangia labda gharama za kuzika ndiyo watachangia," alisema Machicha.

Alisema baada ya kuelezwa hivyo na wananchi alirudi tena Mloganzila kuwajulisha, lakini uongozi wa hospitali hiyo ulimweleza apeleke muhtasari wa mkutano wa wananchi walioketi ili kujiridhisha walivyosema wananchi pamoja na kibali cha mahakama.

Aliongeza kuwa jana kama angekuwa amekamilisha nyaraka zote uongozi wa hospitali hiyo ungekubali kutoa mwili huo ili taratibu za maziko zitafanyika.

"Jana (juzi) nilikwenda kituo cha polisi cha Stakishari kuwaeleza ili kupewa mwili kwa ajili ya kwenda kuzika wasije wakajitokeza watu wengine, lakini polisi walinieleza kwa kuwa suala hili siyo la jinai kawaeleze watu wa ustawi wa jamii ndio wahusika wa suala hilo," alisema.



Askari wa majeshi ya Zimamoto na Uokoaji na Polisi Mkoa wa Morogoro, wakishirikiana kuokoa majeruhi baada ya gari aina ya Coaster kuangukiwa na lori la mizigo katika eneo la Nanenane, jana na kusababisha vifo vya watu wanne na wengine sita kujeruhiwa. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

# Ajali ya Coaster, lori yaua wanne

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

WATU wanne wamefariki dunia na wengine sita kujeruhiwa vibaya, baada ya gari waliloluwa wakisafiria kuangukiwa na kontena la lori la mizigo katika eneo la Nanenane Manispaa ya Morogoro.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Dk. Ritha Lyamuya, alisema alipokea majeruhi kumi ambao kati yao wanne walijeruhiwa vibaya.

Kwa mujibu wa Dk. Lyamuya, majeruhi waliofikishwa wakiwa mahututi walifariki dunia wakati wakipatiwa matibabu.

Dk. Lyamuya alisema kati ya waliofariki dunia wanawake ni wawili na wanaume wawili na kwamba majeruhi waliobaki wanaendelea kupata matibabu katika hospitali hiyo, huku hali zao zikiendelea vizuri kiasi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbrod Mutafungwa, alisema ajali hiyo ilitokea saa 3:30 asubuhi baada ya tela lori la mizigo kukatika na kutenganisha kichwa cha lori hilo na tela lake.

Kamanda Mutafungwa aliitaja gari iliyoangukiwa na lori kuwa ni Coastal yenye namba za usajili T 149 DNZ iliyokuwa ikitokea jijini Dar es Salaam kwenda Morogoro.

Alisema lori hilo lenye namba za usajili T 199 BKW lililokuwa limebeba tumbaku likitokea Moro.

Kamanda Mutafungwa alisema chanzo cha ajali hiyo ni kukatika kwa tela kwenye lori hilo.

# RC akerwa kasi ujenzi

**Na Friday Simbaya,** KILOLO

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, ameelezea kukerwa na kasi ndogo ya ujenzi wa kituo cha afya cha Ruaha Mbuyuni, wilayani Kilolo, hivyo kumtaka mkandarasi kukamilisha kazi hiyo kabla ya mwisho wa mwezi huu.

Hapi alisema hayo juzi wakati wa ziara yake ya kikazi ya kukagua miradi ya maendeleo wilayani Kilolo. Pamoja na mambo mengine, alitoa maagizo kwa mkandarasi huyo kutekeleza kazi katika muda uliopangwa.

Alisema serikali ilishatoa fedha kwa ajili ya ujenzi na kuongeza kuwa hakuna sababu za kuchelewa kukamilisha ujenzi ili wananchi waanze kupata huduma za afya mapema iwezakanavyo. "Sijaridhishwa na kasi ya ujenzi wa kituo cha afya cha Ruaha Mbuyuni kwa hiyo namtaka mkandarasi anayesimamia ujenzi ya kituo hiki pamoja na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, kuharakisha ujenzi huo ili wananchi waanze kupata huduma za afya," alisema.

Kukamilika kwa kituo hicho kilichoko katika Kata ya Ruaha Mbuyuni inayoundwa na vijiji vya Ruaha Mbuyuni, Ikula, Msosa na Mtandika, kutawezesha kutoa huduma kwa wakazi takribani 13,123 na kata za jirani za Nyanzwa na Mahenge.

Pia kukamilika kwa kituo hicho kutasogeza huduma ya afya ya rafani karibu kwa wakazi wa kata hiyo, kusongeza huduma za afya kwa kinamama na watoto na kupunguza vifo kwa wajawazito. Aidha, kukamilika kwa kituo hicho kutasaidia kutoa huduma za dharura hasa zitokanazo na ajali za barabarani ikizingatiwa kata ya Ruaha Mbuyuni iko mkabala na barabara kuu iendayo Mbeya na nchi jirani.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa kituo hicho, Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Kilolo, Jasphone Mukungu, kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya hiyo, Lain Kamendu, alisema jengo la wagonjwa wa nje (OPD) na choo vimeezekwa na kupigwa lipu.

Alisema kwa sasa kazi zinazoendelea ni pamoja na uwekaji vigae, upachikaji fremu za milango kwa baadhi ya vyumba, utengenezaji wa madirisha na milango ya grili na aluminiamu, upakaji rangi na ujenzi wa mashimo ya mfumo wa majitaka.

Mukungu aliongeza kuwa ili kujenga miundombinu yote inayohitajika, gharama za mradi ni Sh. milioni 500 na hadi sasa halmashauri imepokea Sh. milioni 225.7 ikiwamo nguvu ya wananchi Sh. milioni 20.7.

Katika mradi huo, alisema serikali kuu imetoa Sh. milioni 200 na Sh. Milioni tano ni mchango binafsi wa Rais John Magufuli.

Ofisa mipango huyo alifafanua kwa fedha zilizotumika mpaka sasa ni Sh. 191.9 kwa ajili ya ujengo la OPD na kiasi kilichobaki ni Sh. milioni 33.8.

Mukungu alisema kwa mujibu wa ramani za vituo vya afya, miundombinu inayohitajika ili kuwezesha utoaji wa huduma kikamilifu ni jengo la upasuaji, jengo la mama na mtoto, jengo la kuhifadhia maiti, jengo la kutoa huduma kwa watu wenye VVU/Ukimwi na nyumba za watumishi.

# PM: Tanzania ya kwanza Afrika kusambaza umeme

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema Tanzania imeshika nafasi ya kwanza barani Afrika kwa kufanikiwa kusambaza umeme nchini kwa asilimia 80.

"Leo hii Tanzania ni ya kwanza barani Afrika kwa kusambaza umeme kote nchini hadi vijijini na kufikisha asilimia 80. Kuna nchi ngapi barani Afrika, lakini Tanzania imefanikiwa kuwa ya kwanza. Tumeweza kufikia vijiji 9,112 Tanzania na hadi Aprili 2020 tumetumia Sh. trilioni 2.27," amesema. Alitoa kauli hiyo jana, wakati akielezea mafanikio ya serikali kwenye mkutano wa viongozi wa dini kutoka kamati za amani za mikoa mbalimbali Tanzania Bara na Zanzibar, uliofanyika kwenye Kituo cha Mikutano cha Mwalimu Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na viongozi waliohudhuria mkutano huo ulioandaliwa ili kuunga mkono juhudi za Rais Dk. John Magufuli na serikali yake katika ustawi wa amani, uzalendo na kumtanguliza Mungu, Waziri Mkuu alisema ushirikiano mkubwa wanauonyesha kwa serikali, umefanya mambo mengi ikiwamo kuimarisha huduma za upatikanaji wa nishati kwa ajili ya ustawi wa Watanzania.

Alielezea mambo mengine 15 yaliyofanyika kwa ufanisi chini ya uongozi wa Dk. Magufuli ikiwamo kurejesha nidhamu na uwajibikaji katika utumishi wa umma; mapambano dhidi ya dawa za kulevya; ulinzi wa rasilimali za taifa; kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato na kukua kwa uchumi. Mengine ni mapambano dhidi ya umaskini na ukosefu wa ajira; ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya afya; maboresho ya elimu; huduma za maji; ujenzi wa bwawa la kufua umeme la Nyerere, mradi wa reli kwa kiwango cha kimataifa (SGR); usafiri wa anga; ujenzi wa meli na bandari na barabara na madaraja.

Kuhusu kuondoa umaskini na ukosefu wa ajira, alisema kupitia sekta kuu za viwanda, kilimo, biashara, madini, utalii, miundombinu ya kimkakati pamoja na mifumo ya mikopo nafuu, serikali imezalisha ajira za kutosha kwa Watanzania.

"Kupitia ujenzi wa viwanda vipya, tumetengeneza jumla ya ajira 482,601 na utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya SGR, Stieglers' Gorge, ujenzi wa shule, hospitali na ufufuaji wa mashirika yetu tumefanikiwa kutengeneza ajira 6,032,299."

Akitoa wasilisho la viongozi wa dini, Katibu wa Kamati ya Amani, Askofu Jackson Sosthenes, alisema lengo la mkutano wao ni kumpongeza Rais Magufuli kwa hatua iliyofikiwa ambayo Tanzania imefikia kabla ya mwaka 2025, miaka mitano kabla ya muda uliopangwa.

"Viongozi wa serikali ya awamu ya tano wameweza kufikia matarajio ya wengi na wamekuwa siyo watu wa maneno mengi. Siri ya yote hayo ni kumtanguliza Mwenyezi Mungu kama ilivyosemwa kwenye maandiko Matakatifu kwamba mtafuteni kwanza Mungu na mengine yote mtazidishiwa," amesema.

Akitoa tamko la viongozi wa dini, Mwenyekiti wa Kamati ya Amani, Sheikh Alhad Mussa alisema ujasiri wa Rais Magufuli wa kutozuia ibada na kukata kufungia watu ndani (lockdown), ulimpendeza Mwenyezi Mungu na akaamua kuifanya Tanzania kuwa nyota inayong'ara ulimwenguni.

Kuhusu uchaguzi mkuu ujao, Sheikh Alhad alisema: "Viongozi wa dini hatuko tayari kushuhudia uvunjifu wa amani ukitendeka nchini. Tunawaomba viongozi wa saisa wahakikishe wanalinda amani yetu na mshikamano wetu."

Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zubeiry ambaye alikuwa wa kwanza kutoa salamu za viongozi wakuu wa dini, alisema mtu mwenye akili anahitaji pointi ndogo tu kuona kinachofanywa na Rais Magufuli. "Mambo aliyoyafanya Mheshimiwa Rais kwa nchi yetu hayahitaji kufikiri sana kwa sababu yako dhahiri. Amefanya kazi kubwa ndani ya miaka mitano, ambayo yangeweza kufanyika kwa miaka 25."



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa daraja katika eneo la Pugu, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Watumishi NARCO matatani tuhuma upotevu wa ng'ombe

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MKUU wa Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, Onesmo Buselu, ameagiza Jeshi la Polisi kuwakamata watumishi wote wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) West Kilimanjaro, kufuatia kashfa ya kupotea kwenye mazingira ya kutatanisha ng'ombe 17 wa serikali waliokuwa wanatunzwa kwenye ranchi hiyo.

Buselu amesema tangu wizi huo ufanywe, hakuna taarifa yoyote iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo, jambo linaonyesha kuna njama za makusudi zilizowekwa na watumishi hao kuiibia serikali.

Alitoa uamuzi huo jana baada ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, kutembelea Ranchi ya West Kilimanjaro na kupokea taarifa ya kuwapo wizi wa ng'ombe hao wa serikali, huku kukiwa hakuna hatua zozote zilizochukuliwa dhidi ya watumishi waliohusika na wizi huo.

Akizungumza na watumishi wa ranchi hiyo, Waziri Mpina alieleza kutokuridhishwa na hatua zilizochukuliwa na uongozi wa ranchi kuhusiana na kashfa hiyo na kuagiza kuwa ifikapo Jumatano (kesho), mifugo yote iliyopotea iwe imerejeshwa ndani ya ranchi hiyo. Waziri Mpina alisema hatua zilizochukuliwa za kuwasimamisha kazi watumishi wawili kufuatia wizi huo ni njama za kuficha mtandao wa uhalifu huo na kuagiza vyombo vya dola kufanya uchunguzi wa kina ili kuunasa mtandao wote uliohusika katika kashfa hiyo.

Alimwagiza Meneja Mkuu wa NARCO kuwasimamia kikamilifu watumishi wake kusimamia ulinzi wa rasilimali hizo za nchi na kutokuwa sehemu ya kuhujumu na kushiriki vitendo vya wizi.

Akizungumza kwenye mkutano uliofanyika Kijiji cha Miti Mirefu kinachopakana na Ranchi ya West Kilimanjaro pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo West Kilimanjaro, Waziri Mpina alitoa siku 15 kwa wafugaji waliopangisha kwenye maeneo ya (Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI), kulipa deni la Sh. milioni 19 na wakishindwa kufanya hivyo, serikali itavunja mkataba na kuwaondoa kwenye hilo.

Pia, aliagiza TALIRI kuhakikisha ndani ya siku 15 iwe imekarabati josho na wananchi na waanze kuogesha mifugo yao na serikali itapeleka dawa ya ruzuku, huku akiagiza NARCO kukarabati majengo ya TALIRI ili yatumiwe na wananchi hao kama zahanati.

Kuhusu malalamiko ya wafugaji ya kukosa njia ya kupitisha mifugo, Waziri Mpina alimwagiza Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Halmashauri kwa kushirikiana na wananchi na wawakezaji kutengeneza njia ya mifugo ili wafugaji hao kumaliza mgogoro huo.

Alisema serikali inaendelea kuboresha maisha ya wafugaji ndiyo maana imetengeneza kanuni mpya zikiwamo za chanjo ili kuilinda mifugo kwa magonjwa na kuweka bei elekezi za chanjo.

**HABARI KITAIFA**

# Elimu bure yapunguza watoto mitaani

**Na Renatha Msungu,** CHEMBA

SERIKALI imesema mpango wa elimu bila malipo umesaidia kupunguza idadi ya watoto wa mitaani wasiosoma ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Aidha, watoto wanaoandikishwa kuanza kwa ajili ya elimu ya msingi wameongezeka kutoka milioni 10 hadi 12 ndani ya miaka mitano.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Mwita Waitara, alipokuwa akizindua maadhimisho ya Wiki ya Elimu yaliyofanyika kitaifa Chemba mkoani Dodoma.

Alisema hivi sasa kwenye mikoa mbalimbali, takribani wanafunzi wote wako shuleni jambo ambalo linatia moyo.

Waitara alisema ushirikiano unaofanywa na asasi za kiraia na serikali unasaidia kwa kiasi kikubwa kuwahimiza vijana na wazazi kuwapeleka watoto shuleni.

Pia alisema serikali imejikita katika elimu ndiyo maana inashirikiana na asasi za kiraia kuhakikisha elimu inasonga mbele.

"Ninaomba niseme tu awamu hii watoto wasiosoma wamepungua sana mtaani na hii inatokana na elimu kuwa bure," alisema Waitara.

Alisema pia mpango wa chakula shuleni nao umechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza mahudhurio katika shule mbalimbali nchini.

Aidha, Waitara alitoa wito kwa Mtandao wa Elimu Tanzania (TENMET) kushirikiana na serikali kuhakikisha wanaboresha elimu kwani licha ya kutoa Sh. bilioni 24 kama ruzuku kila mwezi bado ushirikiano unahitajika.

"Jambo hili tukilibeba kwa pamoja tutafanikiwa, serikali imechukua hatua kadhaa kuhakikisha ubora wa elimu unaongezeka, ninachoomba tushirikiane mnapokwama tuambieni, "alisema Waitara.

Waitara pia alizishukuru asasi kuendelea kuisaidia serikali katika mambo mbalimbali huku akisisitiza ziendelee kujenga mabweni, madarasa ili kuinua kiwango cha elimu nchini.

Naye Ochola Martini, Mratibu wa TEMET, aliipongeza serikali kwa kuwekeza katika elimu, hivyo wakiwa asasi ya kiraia watakuwa pamoja kuhakikisha wanasonga mbele.

Alisema elimu ni muhimu kwa watoto, hivyo watakuwa pamoja katika kushirikiana na serikali kuhakikisha sekta hiyo inafikiwa mafanikio.

"Tunaiahidi serikali tutakuwa pamoja popote tutakapohitajika hatuwezi kuwaangusha," alisema Wayoga.



Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye (kulia), akizungumza na timu ya maofisa kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kabla ya kuanza kwa kampeni ya wiki mbili ya elimu kwa mlipakodi mkoani humo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CHADEMA yatoa orodha ya tatu wagombea ubunge

**Na waandishi wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimetoa orodha ya tatu ya wagombea wa ubunge kupitia chama hicho katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, wakiwamo wa majimbo matatu yaliyokuwa yamebaki jijini Dar es Salaam.

Orodha hiyo iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Mkuu wa Idara na Mawasiliano wa chama hicho, Tumaini Makene, ilikuwa na majina ya wagombea 11 wakiwamo Sina Manzi aliyepitishwa kuwania ubunge wa Temeke, Hashim Issa (Ilala) na Ernest Mgawe (Kibamba). Makada wengine wa chama hicho waliotuliwa na majimbo kwenye mabano ni: Modestus Chitemi (Kilombero); Ngassa Mboje (Igunga); Mohamed Kamtande (Mchinga); Hamad Kamtande (Liwale); Mwinula Kasonzo (Solwa); Samson Muhembano (Chamwino); Geofrey Kipengele (Kilwa Kaskazini); na Magoma Magoma (Hanang').

Orodha ya kwanza ya wagombea wa CHADEMA ilitolewa na Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA Bara, Benson Kigaila, ikionyesha mageuzi ya kinamama kuchomoza wakiwa jumla ya wateule 40 kati ya 163.

Katika orodha ya pili ilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Makene, kulikuwa na wagombea ubunge 37 katika majimbo ya Tanzania Bara, wakiwamo kinamama 11.

Majina 11 yaliyotolewa jana, yanafanya idadi ya wagombea wa chama hicho kufikia 211 (wanawake 51), hivyo chama hicho bado hakijateua wagombea kwenye majimbo matatu ya Tanzania Bara. Tanzania ina majimbo ya uchaguzi 264. Kati yake, 214 yako Tanzania Bara na 50 yako Zanzibar.

■**Imeandikwa na Magdalena Haule, Mary Mshami, Fatma Mtutuma na Faudhia Sultan.**

# Utitiri wa wagombea urais wamtisha mbunge mstaafu

**Na Thobias Mwanakatwe**

MBUNGE wa zamani wa Jimbo la Kigamboni (CUF), Frank Magoba, amesema utitiri wa wagombea urais kutoka vyama vya upinzani unakipa nafasi Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuibuka na ushindi katika uchaguzi mkuu mwaka huu.

Magoba, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mambo mbalimbali yanayoendelea nchini katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Hadi sasa, vyama 17 vyenye usajili vimesimamisha wagombea nafasi ya urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Magoba ambaye alikuwa mbunge wa jimbo hilo kati ya mwaka 2000/2005, alisema utitiri wa wagombea urais kutoka upinzani unainufaisha CCM.

"Tumeshuhudia hivi karibuni vyama karibu vyote vimeteua wagombea urais, tunapokuwa na utitiri wa wagombea urais kutoka upinzani... tafsiri yake ni kwamba tunainufaisha CCM ili iendelee kutawala miaka hadi miaka," alisema. Aliongeza kuwa hata katika nchi kama Kenya, Malawi na Zambia ambazo wapinzani walifanikiwa kupata ushindi, waliungana na kutwaa madaraka ya nchi.

"Dawa ya kuiondoa CCM ni kuungana, kuaminiana na kuwa wa wazi. Pia nina maana upinzani ukiungana basi wale viongozi watakaoteuliwa kusimamia umoja huo wawe waaminifu kwa wengine watakaokuwa chini yao, kwani bila hivyo bado umoja huo utakuja kugawanyika na kuendelea kupiga 'mark time'," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo, katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu vyama vya upinzani vielekeze nguvu zao kupata viti vingi vya ubunge na udiwani kwa kuwa kufanya hivyo kutavirahisisha kuingia ikulu katika chaguzi zijazo.

"Katika uchaguzi ulio mbele yetu viongozi wa vyama vya upinzani wakae chini na kutafakari kwa sababu naona kabisa hakuna maelewano kati ya vyama na vyama, haviwezi kushinda katika uchaguzi huu, ni lazima wapinzani wajitathmini kama kweli vinaweza kuiondoa CCM madarakani," alisema.

Alisema ni jambo lililo wazi kuwa kutokana na utitiri wa wagombea urais kutoka upinzania kura zitagawanyika, hivyo CCM itashinda kirahisi badala yake vitabaki kulalamika kuwa wameibiwa kura, kumbe wachawi ni wenyewe.

Magoba alisema kinachotakiwa hivi sasa ni kwa vyama vya upinzani kuelekeza nguvu katika majimbo, ili kupata wabunge na kuachia majimbo pale mmoja wa wagombea atakapokuwa anakubalika, vinginevyo watakuwa wanapoteza muda na fedha nyingi bila kupata matokeo mazuri.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# CCM isiwaonee huruma watiania waliojihusisha na vitendo vya rushwa

**YAMEKUWAPO** madai kwamba watiania kadhaa wa nafasi za ubunge ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) walijihusisha na vitendo vya rushwa kabla na wakati wa mchakato wa kuwashindanisha kupitia kura za maoni.

Walalamiko hayo yamekuwa yakitolewa na baadhi ya watiania, wanachama wa CCM na viongozi kadhaa wa chama hicho tawala.

Mbali na tuhuma hizo, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imethibitisha baadhi ya watiania kujihusisha na vitendo vya rushwa, huku ikiwakamata na kuwahoji baadhi yao.

Kwa ujumla yamezungumzwa mengi kuhusiana na matukio yaliyotokea katika mchakato wa kura za maoni. Kuna watu wanaosikika wakidai kuwa fedha zilitembezwa na baadhi yao waliandaa tafrija za chakula kwa wapigakura ambao ni wajumbe wa majimbo kisha 'kuwakatia' posho ili wawakumbuke wakati wa kupiga kura.

Hata hivyo, wanachokisubiri wana-CCM na Watanzania kwa ujumla ni hatua zipi zitakazochukuliwa na chama hicho dhidi ya waliobainika kujihusisha na vitendo vyaq rushwa.

Tayari viongozi kadhaa wa ngazi za juu wa CCM wameshaeleza bila kificho kuwa watiania wote waliojihusisha na vitendo vya rushwa watashughulikiwa bila kujali nafasi zao wala sura zao, ikiwamo majina yao kukatwa hata kama wameshika nafasi za kwanza katika kura za maoni.

Kwa jinsi TAKUKURU ilivyokuwa imejipanga kuhakikisha wote waliobainika kujihusisha na rushwa wanafikishwa mbele ya mkono wa sheria, baada ya kukiachia jukumu hilo chama tawala, tunasubiri kuona hatua zitakazochukuliwa dhidi ya wale wote watakaobainika.

Chama hicho kimesema kuwa kimeanza vikao vya taifa kwa ajili ya kuwapata wagombea ubunge na uwakilishi jijini Dodoma, hivyo tunaamini kuwa kimeshapata ushahidi wenye vielelezo vya kutosha kuhusiana na kilichotokea katika mchakato mzima wa kura za maoni.

Bila shaka kamati za maadili za CCM zitakuwa zimekusanya ushahidi mzito na wa kutosha na usioacha shaka kuhusiana na mchakato wa kura za maoni nchi nzima ili uamuzi utakaofanyika kwa haki bila kumuonea mtu yeyote.

Kadhalika, TAKUKURU pamoja na kuliacha suala hilo kwa CCM, lakini tunaamini kuwa kama chombo chenye mamlaka ya kupambana na kuzuia rushwa nchini, itatoa ushirikiano wa karibu kutokana na kuhusika kwa kiwango kikubwa katika mchakato huo.

Tunaamini hivyo kwa kuwa taasisi hiyo iliwatia mbaroni watiania kadhaa na kuwahoji kuhusiana na matukio mbalimbali, ingawa haikuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.


Ni matarajio yetu kuwa majina ya watiania wote yatapitiwa kwa kina na wale waliopata ushindi halali na usio na shaka yoyote wateuliwa na chama hicho kupeperusha bendera yake katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu. Watakaobainika kuwa walitumia fedha kuwahonga wajumbe tunatarajia kuona wakikatwa, na ikiwezekana hatua zaidi za kinidhamu zichukuliwe dhidi yao.

Hatua hiyo itatoa fundisho kwa wanachama wa chama hicho kuwa uongozi sio wa kununuliwa bali unatafutwa kwa njia halali za ushindani kwa lengo la kuwa watumishi wa wananchi.

Kwamba anayeusaka uongozi kwa njia ya fedha hana lengo la kuwatumikia wananchi na kuliletea maendeleo taifa, bali kutetea maslahi yake na kujiletea maendeleo binafsi.

Tunashauri kwamba hatua za kudhibiti rushwa ya uchaguzi ziwapo na ziwe endelevu katika vyama vyote vya siasa kwa kuwa uongozi ni dhamana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kwa juhudi hizi vikwazo kwa mabinti vitamalizika

**MIMBA** na ndoa utotoni ni miongoni mwa matatizo yanayochangia kukwamisha malengo ya kielimu ya wanafunzi wa kike katika mikoa mingi nchini.

Hali hiyo inasababisha upatikanaji wa elimu kwa wote kukabiliwa na changamoto ndiyo maana ushirikiano wa wadau kumaliza kikwazo hicho cha maendeleo ya elimu kwa mtoto wa kike ni suala la kipaumbele.

Wadau wanaohusika katika hili ni pamoja wazazi, walezi na jamii kwa ujumla, ambao kwa pamoja wanatakiwa kuwa mstari wa mbele kupambana kwa kila njia badala ya kujiweka pembeni.

Kushiriki katika mapambano haya kutasaidia kuimarisha hatua mbalimbali, ambazo Tanzania imefikia kwenye kuboresha elimu, ikiwamo kuanzisha na kuongeza shule za msingi na sekondari.

Ikumbukwe serikali inagharamia elimu ya msingi hadi kidato cha nne, ikiwa ni fursa kwa kila mtoto kupata elimu hivyo kikwazo kinachowakabili wanafunzi wa kike hakina budi kumalizwa.

Lakini, kuwapo kwa taarifa za mimba na ndoa za utotoni kwa baadhi ya wanafunzi katika maeneo mbalimbali nchini, ni changamoto kwa maendeleo ya elimu kwa kundi hili.

Dunia ya leo, ili mtu aweze kuboresha maisha yake ni muhimu awe na elimu, kwa kuwa ndiyo inayomwezesha kujitambua na kujimiliki mwenyewe kuendesha maisha yao.

Elimu pia inamfanya mtu kuzikabili changamoto zinazomsonga, katika maisha yake ya kila siku na kuyatawala na kuyatumia mazingira yanayomzunguka, ili kuboresha maisha yake.

Ni vyema ikaeleweka kuwa, wasichana wanaokatisha masomo na kuharibiwa maisha yao, wamo ndani ya jamii na ni sehemu ya Tanzania, hivyo kila mmoja ahusike katika kukomesha mimba na ndoa za utotoni.

Kwa hali hiyo, wazazi na walezi wazungumze na kuwaelekeza, kuwafundisha maadili mema wakiwa wadogo, ili yawe ngao yao ingawa inawezekana wakayaacha, lakini ni muhimu mzazi kutimiza wajibu wake.

Suala la elimu ya makuzi, ni miongoni mwa majukumu ya wazazi na walezi, lakini jamii nayo haipaswi kuwa kimya inapoona mtoto wa kike anafanyiwa ukatili ama anajihusisha na vitendo hivyo.

Elimu hiyo wasiachiwe walimu tu, eti kwa sababu wanakaa na wanafunzi kwa muda mrefu, bali ni jukumu la wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kila upande kufanya sehemu yake, katika malezi bora.

Kila upande utimize wajibu, ili iwe rahisi kuwaepusha na tamaa, ambazo baadaye zinawasababishia kujiingiza katika vitendo vya ngono na kujikuta wakipata mimba ama kulazimishwa kuolewa ndoa za utotoni. Umaskini unatajwa kama sababu mojawapo ya mimba na ndoa za utotoni, lakini ninaamini kwamba, wazazi na walezi wakiamua kuwaelimisha watoto wao watasaidia kupunguza tatizo hilo.

Haipendezi mzazi au mlezi kushirikiana na watu wanaowapa watoto mimba kwa kumalizana kimya kimya nyumbani, badala yake waiachie sheria kuchukua mkondo wake ili kukomesha tatizo hilo. Tayari serikali imekuja na mikakati kadhaa ya kukabiliana na tatizo hilo ikiwa ni pamoja na kukamilisha mwongozo wa kuimarisha na kumaliza vitendo vya mimba shuleni kuanzia mwaka huu wa 2020.

Kwa mujibu wa Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (anayeshughulikia elimu), Gerald Mweli, baada ya kukamilika kwa mwongozo huo wataanza kutoa mafunzo maalumu kwa walimu wawili kila shule, jinsi ya kuendesha elimu hiyo hususani kwa wasichana wanapoanza kupevuka.

Hivyo wakati serikali ikiwa na mikakati hiyo, wazazi na walezi hawana budi kufanya sehemu yao, ikiwamo na kutokubali kushirikiana na wabakaji na mafataki, badala yake linapotokea tatizo, vyombo husika vipewe taarifa.

Naibu Katibu Mkuu, anasema walimu wawili kila shule watafunzwa ili kuhakikisha mabinti wanapatiwa elimu jinsi ya kuepuka vishawishi na kujilinda ili kumaliza mimba za utotoni na kukatishwa masomo yao.

Mbali na mkakati huo, mwingine ni ujenzi wa mabweni na kwamba hadi sasa mabweni yaliyojengwa nchi nzima asilimia 90 ni ya wanafunzi wa kike, hivyo bado juhudi zinaendelea kwa ajili ya kukamilisha hilo.

MAKALA MAALUM

# GPSA ilivyookoa mamilioni ununuzi serikalini

## ■Samani shuleni sasa wazipata bei ya jumla
## ■Ununuzi, matumizi petroli 'yakabwa hadi kona'
## ■Serikali yachekelea ushindi gawio Sh. mil. 900

**Na Enock Charles**

SASA hivi kitaifa na kimataifa, dhana ununuzi na utunzaji vifaa ambayo kimsingi ni taaluma inayoshika kasi kimataifa, ina thamani na hadhi sawa kama ilivyo fedha ambayo unyeti wake ni mkongwe.

Kwa hatua iliyofikiwa nchini, taaluma hiyo ina bodi maalum inayosimamia maendeleo yake kama ilivyo kwa wahasibu, huku serikalini nako kukiwa kumezama kwa sura ile ile ya uhasibu, kukiwapo wakala na vyombo mbalimbali vinavyosimamia eneo hilo.

Aidha, ili mhasibu nchini atimie kwa sifa ya juu kwenye taaluma yake, anatakiwa awe na cheti kiitwacho 'Certified Public Accountant', au kwa umaarufu wake CPA, wanunuzi na watunzaji vifaa wao wana yao iitwayo 'Certified Supplies and Procurement', maarufu CSP. Taaluma hiyo ya ununuzi, inamkumbusha yule anunuaye bidhaa jicho lake la kwanza liwe katika mambo matano makuu ambayo wenyewe huyaita '5Rs' (five rights) ambayo ni usahihi katika; bei, idadi ya bidhaa, ubora wake, muda na chanzo.

Katika kutekeleza hizo 5Rs daima zisikosewe ila ziboreshwe, serikali ina mdau wake anayeitwa Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA), wenye mzizi wa kihistoria unaoanzia mwaka 1997, pale iliposimikwa sheria maalum ya kuuhalalisha na kisha ikafanyiwa maboresho mnamo Desemba 7, 2007.

Hata hivyo, uhai wake kamili wa kiutendaji, ulishuhudiwa pale ulipozinduliwa rasmi Juni 16, 2008, kipindi hicho ukijulikana kama Bohari Kuu ya Serikali, ukiwajibika chini ya Wizara ya Fedha.

**KAULI YA CEO**

Ofisa Mtendaji Mkuu wa GPSA, Profesa Geraldine Rashel, anasema asilimia 70 ya bajeti ya serikali inaangukia kwenye ununuzi wa mahitaji na huduma mbalimbali, katika sura za bidhaa, kandarasi na huduma.

Profesa Rashel anasema GPSA ni kiungo muhimu katika ukuzaji wa biashara nchini na kimataifa, akitaja malengo ya kuanzishwa kwake ni kuipunguza gharama serikali, upatikanaji wa vifaa na huduma bora, kuchochea ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini.

Anataja baadhi ya maeneo ambayo wakala unawajibika kwa kiasi kikubwa ni kwenye kutoa huduma ya vifaa vya ofisi na mafuta ya magari kwa serikali na taasisi zake, huku pia ukiwa na nafasi ya kitaaluma katika kugomboa mizigo ya serikali bandarini, viwanja vya ndege na mipakani.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, majukumu mengine ya wakala ni kutoa uhifadhi salama wa vifaa na mali za taasisi za umma kitaalamu, ununuzi wa pamoja wa magari ya serikali, kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za ununuzi, ugavi na ugomboaji mizigo, kuandaa na kutoa orodha ya wazabuni wa vifaa na huduma mtambuka (VHM).




Sehemu ya aina ya majengo ya serikali, yanayotajwa GPSA kuwa na mkono wake katika kudhibiti bajeti na kusimamia ubora unaostahili. **PICHA: MTANDAO**

**ELIMU BURE**

Profesa Rashel anasema wakala umechangia kiasi cha Sh. milioni 900 katika mfuko mkuu wa serikali kwa mwaka wa fedha 2019/20 na umekuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji wa mpango wa serikali wa kutoa elimumsingi bila malipo, maarufu elimu bure.

"Wakala umeanza kununua vifaa vya shule za msingi na sekondari kwa bei ya ushindani ili kuipunguzia gharama serikali katika kutekeleza mpango wa elimu bure," anasema.

Anabainisha kuwa wakala unatoa huduma ya uhifadhi wa vifaa na mizigo ya taasisi za serikali zinapokuwa na uhitaji na wakati wa majanga mbalimbali, akitolea mfano walivyohifadhi vifaa na mizigo ya serikali wakati wa tetemeko la ardhi mkoani Kagera mwaka 2017.

Profesa Rashel pia anasema wakala umeisaidia serikali katika kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo (1999-2025) na mpango wa kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye uchumi wa kati unaochagizwa na viwanda, kwa kutoa kipaumbele kwa wazalishaji wa ndani kupata soko kwa kuzihudumia taasisi za serikali.

Akifafanua zaidi kuhusu hoja hiyo, kiongozi huyo anasema anawataja wazalishaji wa ndani walionufaika kuwa ni pamoja na Maswa Group Limited wanaozalisha chaki mkoani Simiyu na Lyanzile Company wanaozalisha 'green tags'.

MAFUTA YA MAGARI

Profesa Rashel anabainisha kuwa wakala kwa sasa unatoa huduma ya mafuta ya magari na vifaa katika mikoa 23 Tanzania Bara (mikoa mipya ya Njombe, Simiyu na Geita haina huduma hiyo) na unauza vifaa vya ofisi kwenye taasisi za serikali katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

Anasema wakala umeboresha muda wa kutoa huduma ya mafuta, akibainisha kuwa magari ya serikali yanapata huduma hiyo katika vituo vyake vyote kuanzia saa 1.30 asubuhi mpaka saa 12 jioni kila siku zikiwamo za mwishoni mwa wiki na hata sikukuu za kitaifa.

"Kwa mafanikio makubwa, wakala ulitoa huduma ya mafuta kwa ufanisi kwa magari ya taasisi, mashirika na viongozi wa ukanda wa SADC wakati wa mkutano wa 39 mwaka 2019," anasifu.

**UNUNUZI WA MAGARI**

Profesa Rashel anasema kiasi kikubwa cha fedha kimeokolewa kutokana na mchakato wa ununuzi na punguzo kubwa linalopatikana kutokana na ununuzi wa pamoja.

Anasema wakala pia umekuwa kituo maalum (one stop centre) kwa ajili ya ununuzi wa magari ya serikali kwa kutoa taarifa zote zinazohusu magari, watengenezaji na wazabuni, hivyo kuongeza uwazi na utawala bora katika eneo hilo la ununuzi wa magari ya serikali.

"Wakala pia umefanya mabadiliko makubwa katika eneo hili ambapo taratibu nyingi (local operations) zitafanywa na wakala ikiwamo kulipia moja kwa moja kwa watengenezaji wa magari ili kupunguza gharama ya uwapo wa mtu wa kati," anasema.

**ORODHA WAZABUNI**

Profesa Rashel anasema wakala una jukumu la kufanya mchakato wa kutafuta wazabuni wa bidhaa na huduma mtambuka kwa niaba ya taasisi za umma.

Katika kutekeleza jukumu hilo, kiongozi huyo anasema utaratibu huo umesaidia kuokoa gharama za michakato ya zabuni kwa taasisi za umma kila zinapohitaji huduma na vifaa mtambuka (common use items and services), huku wakala ukitoa fursa kwa wazabuni na taasisi binafsi kufanya biashara na serikali.

"Kwa mwaka huu wa fedha 2020/21, mchakato unafanyika kupitia katika mfumo wa kidigitali wa ununuzi wa umma unaoitwa kitaalamu 'TANePS' unaomtaka kila mzabuni atakayeshiriki kujisajili na kupata kwanza akaunti na nywila (password).

**UGOMBOAJI SHEHENA**

Profesa Rashel anasema wakala umegomboa mizigo kwa niaba ya taasisi za serikali kwa usalama, uhakika na gharama nafuu, akifafanua kuwa mafanikio hayo yametokana na uzoefu na weledi mkubwa wa watumishi wa wakala pamoja na uwekezaji na uboreshaji mkubwa wa miundombinu katika eneo la ugomboaji na uondoshaji mizigo.

"Baadhi ya kazi zilizofanyika kwa ufanisi ni pamoja na ugomboaji mizigo ya taasisi, mashirika na viongozi na marais wa ukanda wa SADC wakati wa mkutano wa 39 mwaka 2019. Wakala umeongeza wigo wa huduma hii kwa taasisi zote za umma na miradi mikubwa ya serikali," anatamba.

**HIFADHI YA MAFUTA**

Kuhusu mipango na mikakati ya wakala huo, Profesa Rashel anabainisha kwamba wataendelea kuagiza vifaa kutoka kwa wazalishaji wa ndani na nje ya nchi, ili kuvipata kwa nafuu zaidi kutokana na kukwepa gharama za mtu wa kati na pia punguzo kubwa la bei kutokana na kununua vifaa kwa wingi (bulk purchase) na kulipa fedha taslimu (cash discount).

Anasema wakala pia utazidi kusogeza huduma kwa wateja wake mpaka ngazi ya wilaya, akibainisha kuwa mpaka sasa, wakala umefungua ofisi ndogo katika wilaya za Ileje mkoani Mbeya na Kahama mkoani Shinyanga na wako katika mkakati wa kujenga ofisi wilayani Mafinga mkoani Iringa.

"Wakala utaendelea kufanyia maboresho na kujenga miundombinu yake ikiwamo ya kuhifadhi mafuta yatakayonunuliwa moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji.

"Lengo ni kununua mafuta kwa bei rahisi, hivyo kuziuzia taasisi za umma kwa bei ya chini zaidi ya soko itakayopunguza gharama za uendeshaji kwa taasisi za umma," anasema.

# Fursa zarejea Kagera ujio wa MV Victoria

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WAKAZI wa Mkoa wa Kagera wametakiwa kufanya kazi kwa bidii ili wanufaike na uwapo wa meli ya New Mv. Victoria Hapa Kazi tu iliyoanza kazi rasmi na kupokelewa mjini Bukoba jana ikitokea mkoani Mwanza.

Meli hiyo ilikuwa ikifanyiwa ukarabati mkubwa kwa takriban miaka sita.

Akizungumza baada ya meli hiyo kuwasili katika Bandari ya Bukoba, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe alisema meli hiyo imekarabatiwa kwa gharama ya Sh. bilioni 22.7, na kuwasisitiza wananchi kujituma katika shughuli za uzalishaji mali ili kujiinua kiuchumi kupitia usafiri huo.

"Nimepanda meli kwa mara ya kwanza, lakini sikuchoka, nimelala kama niko nyumbani, tumetoka Mwanza na abiria 301 pamoja na mizigo yao," alisema na kuongeza:

"Hizi ni jitihada za serikali ya awamu ya tano kuhakikisha inaboresha mazingira ya usafiri na usafirishaji, wananchi ungeni mkono jitihada hizi kwa kuitunza, lakini mkiendelea kunufaika kwa kusafirisha mizigo yenu kwa gharama nafuu."

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, alisema meli hiyo ilipositisha safari za Bukoba mji ulilala na kuwa sasa utachangamka kibiashara na mzunguko wa fedha utakuwapo, maana watu zaidi ya 2,000 watakuwa kazini kwa saa 24.

"Wafanyabiashara, mama lishe, bodaboda na wengine watakuwa kazini hadi usiku na mji utachangamka kibiashara, ni mikoa michache ambayo inaweza kutumia usafiri wa aina tatu kwa wakati mmoja, wanaohitaji usafiri wa anga ndege zipo, wa nchi kavu magari yapo, lakini sasa hata meli yetu imerejea kwa ajili ya watakaohitaji kutumia usafiri wa majini," alisema Gaguti.

Alisema kwa sasa mizigo mingi itaingia na kutoka kwa gharama nafuu, na kuwa mizigo inayotoka Bukoba kwenda Mwanza tani moja ni zaidi ya Sh. 100,000 kwa magari, lakini kwa meli ni chini ya Sh. 30,000.

"Bidhaa zinazozalishwa Kagera zitakuwa na bei nafuu katika masoko kutokana na gharama za usafirishaji kushuka, lakini pia zinazoingia Kagera hasa za viwandani zitashuka bei, na kuwafanya wananchi kupata unafuu wa maisha," alisema Gaguti.

Baadhi ya wananchi waliozungumza na Nipashe akiwamo Godfrey Leonidas mkazi wa manispaa ya Bukoba, waliomba serikali kupunguza nauli ya daraja la tatu kutoka Sh. 16,000 hadi 12,000 kutokana na hali ya uchumi kwao kwa sasa kuwa ngumu.



Wananchi wakiangalia gari aina ya Toyota IST, lililopata ajali baada ya kugongana na basi la BM Coach, katika eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana. Abiria wanne waliokuwa kwenye gari hilo, walitoka salama. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Waziri: Sekta ya nishati ni 'uti wa mgongo' wa uchumi

**Na Hafsa Omar,** NGARA

NAIBU Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, amesema sekta ya nishati ina nafasi kubwa kuziwezesha sekta nyingine zifanikiwe kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mgalu alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa ziarani kukagua usambazaji umeme vijijini katika wilaya za Ngara na Biharamulo mkoani Kagera.

Katika ziara hiyo, Mgalu aliwasha umeme katika taasisi za umma ambazo ni vituo vya afya na shule za sekondari.

Alisema sekta zote zinategemea nishati ya umeme, akitolea mfano sekta ya afya ambayo ina vituo vya afya na zahanati ambazo zimeunganishiwa nishati hiyo, hivyo kuwawezesha wananchi kupata huduma kwa urahisi.

Akiizungumzia sekta ya elimu, naibu waziri huyo alisema kiwango cha ufaulu nchini kimeongezeka hasa katika maeneo ya vijiji kutokana na kazi nzuri ya usambazaji umeme vijijini.

Mgalu alimtaka mkandarasi wa mkoa huo kuendelea kusambaza umeme katika maeneo ambayo yamesalia kwa kuwa mradi huo upo ukingoni na wananchi wa vijiji hivyo wanahitaji huduma hiyo.

Pia, aliwatoa hofu wananchi mkoani hapa kuhusu upatikanaji wa umeme, akisisitiza kuwa serikali itahakikisha upatikanaji wake unakuwa wa uhakika wakati wote.

"Serikali inatekeleza miradi mikubwa miwili ya umeme inayojenga njia ya kusafirisha umeme na vituo vyake, mradi mmoja ni Bulyanhuru-Geita ya njia ya kusafirishia ya msongo wa Kv 220 na mwengine Geita-Nyakanazi wa msongo wa Kv 220, miradi yote inatarajiwa kukamilika mwakani," alisema.

Mganga wa Kituo cha Afya Bukiriro, Dk. Wilbroad Bukiriro, aliishukuru serikali kwa kupeleka umeme kwenye kijiji hicho na kuwezesha kituo cha afya kupata nishati hiyo iliyokosekana tangumm kuanzishwa kwake mwaka 1977.

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
(COMMERCIAL DIVISION)
AT DAR ES SALAAM

COMMERCIAL CASE NO. 23 OF 2020

STANBIC BANK TANZANIA LIMITED.............................................PLAINTIFF

VERSUS

DEOGRATIUS BONIPHACE KIGALU.......................................... DEFENDANT

SUBSTITUTED SERVICE BY PUBLICATION

TO:
DEOGRATIUS BONIPHACE KIGALU,
TEGETA WAZO HILL,
KISANGA STREET,
P.O.BOX 33390,
DAR ES SALAAM.

**TAKE NOTICE** that the plaintiff has instituted a suit against you with particulars set out in the plaint filed in this court. Service of the summons on you has been ordered by means of this publication.

You are directed to collect copies of the summons and plaint from the Court's Registry, P.O.Box 12533, Dar es salaam. You are ordered to file your written statement of defence within twenty one (21) days of publication of this notice. You are hereby summoned to appear in this Court in person or by an Advocate or an agent duly authorized on 15th day of September, 2020 at 11:00 am when this case will be heard.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT** should you default to file your written statement of defence and/or enter appearance as herein provided, the suit will proceed and a decision may be given in your absence.

Given under my hand and the seal of the Court this 10th day of August, 2020.

THE HIGH COURT OF TANZANIA ★ COMMERCIAL DIVISION

DEPUTY REGISTRAR

# Ujenzi wa flowmeter wagharimu bil. 47/-

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Bandari Tanzania (TPA), imetumia zaidi ya Sh. bilioni 47 kwa ajili ya mradi wa 'flowmeter' za kuhifadhi mafuta katika bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara.

Akizungumza katika ziara ya kukagua miradi ya uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, alisema lengo ni kuwa na uhakika wa upatikanaji wa mafuta kwa bei nafuu kwa wananchi nchini.

"Nilipoteuliwa nilikuwa naangalia mahesabu ya lita moja ya mafuta yanayouzwa kwa mwananchi wa kawaida, bei ilikuwa kubwa, nikaja bandarini kuuliza kwa nini bei inakuwa kubwa, nikabaini kwamba kulikuwa na changamoto mbili kubwa na ndiyo maana ilibidi tulishughulikie hili," alisema Kamwelwe.

"Sehemu kubwa ya matangi yamekuwa ni ya watu binafsi, kwa hiyo tukaona kwamba ili kuondokana na hili ni lazima tuwe na matangi yetu, na sasa tunakamilisha usanifu wa kujenga makubwa ya serikali ambayo yatahifadhi mafuta yanayotoka kwenye meli na watu wengine watachukua kutoka kwetu."

Kamwelwe alisema zabuni tenda ya kujenga matangi hayo imeshatangazwa.

"Pia mafuta yalikuwa yanapanda bei zaidi kwa sababu meli ilipokuwa inakuja kushusha mafuta badala ya kukaa siku tano, ilikuwa inakaa muda mrefu zaidi na hapo kila siku iliyokuwa ikizidi... tulikuwa tunamlipa mwenye meli kwa hiyo ili kufidia hiyo hasara, alikuwa anatwishwa mzigo mwananchi," alisema Kamwelwe.

"Serikali tuliona hilo halifai na hatuwezi kuendelea kumuonea mwananchi, kwa hiyo kwa kujenga hii mitambo na matangi makubwa, meli haitafika tena siku tano, itakuta mafuta yameshapakuliwa, kwa hiyo hakutakuwa na mahesabu tena ya fidia na hasara tena kwa mwananchi."

"Na ndiyo maana tunaweka nguvu zaidi katika kukarabati bandari ili meli nyingi ziingie zikiwamo hizi za mafuta ya aina zote ambayo yatakuwa yanahifadhiwa hapa."

Alisema mwishoni mwa Oktoba mwaka huu, ujenzi wa mitambo hiyo utakuwa umekamilika.

Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Deusdedit Kakoko, alisema kuwekwa kwa mitambo hiyo kutasaidia kwa kiwango kikubwa kuondoa udanganyifu uliokuwa ukifanywa na wafanyabiashara kwa kushirikiana na watumishi wachache kwenye taasisi za umma.

HABARI KITAIFA

# Maadili ya uandishi wa habari yahimizwa

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WANAHABARI nchini wamehimizwa kuandika habari mbalimbali zikiwamo za uchaguzi wakiepuka vichocheo vya machafuko kwa kuzingatia maadili, sheria na kanuni zilizopo kwenye taaluma.

Mkufunzi wa masuala ya habari kutoka Mtandao wa Redio za Kijamii Tanzania (TADIO,) Rose Haji Mwalimu, alisema hayo alipokuwa akizungumza na mameneja wa redio 35 nchini waliokuwa wakipewa mafunzo ya kuripoti habari bila migongano yaliyofadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kupitia mradi wa SDC.

Alisema wanahabari wanapaswa kutumia vizuri kalamu zao katika kuelimisha na kuburudisha jamii na kwamba kinyume cha hapo, anaweza kufikishwa mahakamani, huku chombo chake cha habari kikifungiwa.

Haji alisema kwa kufuata taaluma inavyotaka na kuzingatia maadili, mwandishi anapaswa kuandika habari kwa kulichambua tatizo badala ya kuandika tatizo lililopo tu, jambo litakaloleta shida ya kiuandishi na kutikisa taaluma.

Alisema kama chombo cha habari kinayo nafasi ya kuangalia namna ya kumaliza tatizo kwa kuandika ukweli kwa kuzingatia mila, tamaduni na dini ili kuepuka migogoro.

Hivyo aliwashauri wanahabari kuhakikisha wanazijua vizuri sheria za haki za binadamu.

Mratibu wa TADIO, Cosmas Lupoja, alisema lengo la semina hiyo ni kuwawezesha mameneja kuzijua sheria za vyombo vya habari na kuzisimamia ili kuepuka kupokea na kutoa habari zenye migogoro na kuhakikisha haziendi hewani.

Meneja wa Redio Uyui ya Mjini Tabora, Saidi Mmanga, alisisitiza wanahabari kuzingatia kanuni za kuripoti habari hasa za uchaguzi ambazo mara nyingi zimekuwa na vitisho kuanzia uchaguzi wa vyama vingi wa mwaka 1995.

# Wataka wagombea uongozi kupimwa akili

**Na Christina Haule,** MOROGORO

SERIKALI imeshauriwa kuingiza kwenye mabadiliko ya kisera au kikatiba suala la sifa ya mgombea kuwa na akili timamu kwa kuwapima kitaalamu zaidi kabla ya kuwachagua.

Hatua hiyo inalenga kumpata kiongozi bora na kuondoa utata wa sifa hiyo ambao umegubikwa na maswali mengi kwa jamii.

Waandishi wa habari kutoka mikoa ya Morogoro na Pwani walitoa ushauri huo jana kwenye mafunzo ya kuripoti habari za uchaguzi kwa kuhimiza ushiriki wanawake katika uongozi, yaliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP-Mtandao) na kufanyika mjini hapa.

**Ipo haja kwa wanahabari kuandika habari zinazoshawishi wanawake kushiriki kwenye uongozi ili kuleta usawa wa kijinsia.**

Mmoja wa waandishi, Thadei Hafigwa, alisema utata uliopo juu ya sifa hiyo mojawapo ya mgombea kuwa na akili timamu ni moja ya utata ambao unafanya jamii kutoelewa zaidi na kwamba ni bora kungewekwa sera ya kutambua kitaalamu akili za mgombea kwa kumpima na vipimo.

Hafigwa alisema licha ya kwamba kwa sasa hakuna kipimo maalum bali ni macho tu hutumika kutambua akili za mgombea, wakati suala la uchunguzi kitaalamu lingewekwa ili kuondoa utata na maswali ya wananchi hasa pale kiongozi anapobadilika mbele yao.

Naye mwezeshaji wa mafunzo hayo, Hawa Mushi, alisema ipo haja kwa wanahabari kuandika habari zinazoshawishi wanawake kushiriki kwenye uongozi ili kuleta usawa wa kijinsia.

Alisema kutokana na ukweli uliopo kuwa nafasi ya wanawake imebanwa katika nyanja mbalimbali ikiwamo kisiasa, kiuchumi na hata kisera wanahabari hawanabudi kuweka msukumo wa wanawake kushiriki kikamilifu katika kuleta msukumo wa masuala ya wanawake.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angella Kairuki (katikati), akikabidhi msaada wa kompyuta kwa Mwenyekiti wa Kituo cha watu wenye ulemavu wasioona cha VIMDATI, uliotolewa na msamaria mwema, Najat Said (kulia), jijini Dar es Salaam juzi. Msamaria huyo pia alitoa vitu mbalimbali zikiwamo samani za ofisi ya kituo hicho na chakula. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# NMB yatengea wachimbaji wadogo bilioni 32/-

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

BENKI ya NMB imetenga Sh. bilioni 32 kwa ajili ya mikopo kwa wachimbaji wadogo nchini.

Akizungumza jijini Mwanza juzi wakati wa kongamano la NMB Business Club, Mkuu wa Idara ya Biashara wa benki hiyo, Alex Mgeni, alisema kutolewa kwa mikopo hiyo ni matokeo ya maboresho ya sheria na sera kwenye sekta ya madini yanayofanywa na serikali kwa lengo la kuongeza tija.

"Mikopo hiyo ambayo imeanza kutolewa tangu Januari, mwaka huu itahusisha gharama za kununua vifaa vya uchimbaji ikiwamo mitambo na magari ya kubebea mchanga wa madini migodini," alisema Mgeni.

Kuhusu madhara ya janga la corona kwa sekta ya biashara, Mgeni alipongeza juhudi za serikali zilizofanikisha kutokomezwa kwa ugonjwa huo uliosababisha changamoto katika mfumo wa biashara na uwekezaji.

Alisema kutokana na mifumo ya biashara kupata changamoto, NMB iliwasaidia wateja wake ambao biashara zao ziliathirika zaidi, hasa wale wa sekta ya utalii.

"Kila mfanyabiashara aliyepata changamoto na kutufikia tulizungumza naye kutafuta namna ya kumsaidia. Wapo waliopunguziwa viwango vya marejesho na wengine marejesho yao yalisimamishwa kwa muda, hasa wale wa sekta ya utalii walioathirika zaidi," alisema.

Mwenyekiti wa NMB Business Club mkoa wa Mwanza, Albert Kassa, aliwataka wafanyabiashara na wajasiriamali nchini kuacha kugeuka wachuuzi wa kununua na kuuza bidhaa, badala yake wajikite kwenye kuzalisha na kuongeza thamani ya bidhaa ili kupata tija zaidi.

"Kwa kuchakata na kuongeza tija badala ya kuuza bidhaa ghafi kutaongeza siyo tu pato la mfanyabiashara mmoja mmoja, bali pia kutatoa fursa za ajira kwa vijana nchini," alisema Kassa.

Alisema kuongezeka kwa pato la wafanyabiashara na fursa za ajira kwa vijana kutatanua wigo wa makusanyo ya fedha za serikali kupitia kodi na ushuru mbalimbali na hatimaye kuongeza uwezo wa serikali wa kugharamia na kuboresha huduma za kijamii katika sekta za afya, miundombinu, maji na elimu.

Akizungumzia NMB Business Club, Meneja wa Kanda ya Ziwa wa Benki hiyo, Baraka Ladislaus, alisema kongamano hilo linatoa fursa kwa benki kusikiliza, kupokea na kufanyia kazi hoja za wateja.

"Kupitia hoja na mrejesho kutoka kwa wateja wetu wafanyabiashara, NMB tunapata fursa ya kuboresha huduma na bidhaa zetu," alisema Ladislaus.

Mfanyabiashara, Contilda Magweti wa jijini Mwanza, alisema licha ya kuwakutanisha pamoja wafanyabiashara, kongamano hilo la kila mwaka pia huwapa fursa ya kukutana na kujadiliana uso kwa uso na viongozi na watendaji wa benki.

"Kwa kukutana pamoja tunapata fursa ya kujadiliana na kubadilishana uzoefu kibiashara; NMB iangalie uwezekano wa kongamano hili kufanyika angalau mara mbili kwa mwaka," alisema Magweti.

# Bil. 100/- sasa kupeleka umeme pembezoni ya miji

**Na Veronica Simba,** ARUSHA

SERIKALI imetenga shilingi bilioni 103.8 kwa ajili ya kupeleka umeme katika maeneo yaliyo pembezoni mwa majiji, mikoa, manispaa na miji, nchi nzima.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alibainisha hayo kwa nyakati tofauti juzi alipokuwa katika ziara ya kazi wilayani Arusha.

Akizungumza kabla ya kuwasha umeme katika Shule ya Sekondari Moivaro na baadaye Shule ya Sekondari Nyahiri Terrat, Dk. Kalemani alisema kuwa serikali inaendelea kuwaunganishia umeme wananchi wa maeneo ya aina hiyo nchini kote kwa gharama ya shilingi 27,000 tu kama ilivyo kwa vijijini.

**Mpango wa serikali ni kutokana na uhalisia kuwa maeneo hayo kwa kiasi kikubwa yanashabihiana na yaliyoko vijijini...**

Alisema mpango wa serikali ni kutokana na uhalisia kuwa maeneo hayo kwa kiasi kikubwa yanashabihiana na yaliyoko vijijini, ambapo asilimia kubwa ya wakazi wake wana kipato kidogo.

"Tulikaa tukaona maeneo haya yaliachwa muda mrefu bila kuwa na miundombinu ya umeme. Tukaona tuwapunguzie gharama kutoka mlivyokuwa mnalipa zamani shilingi 177,000 na katika baadhi ya maeneo 380,000 hadi shilingi 27,000 tu."

Akizungumzia Wilaya ya Arusha, Waziri Kalemani alisema kuna mitaa takribani 26 iliyo pembezoni mwa mji, na kwamba serikali ilianza kuipelekea umeme kutoka mwaka 2018.

Alimpongeza Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Arusha, Mhandisi Herin Muhina, kwa kazi nzuri anayoifanya na kumwagiza atumie muda wa miezi mitatu kuanzia sasa kukamilisha kazi ya kupeleka umeme katika mitaa yote iliyo pembezoni mwa mji, ambayo haijafikiwa na huduma hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Kenan Kihongoji, alimpongeza Waziri Kalemani kwa uchapakazi wake hususan katika kuhakikisha wananchi wa maeneo mbalimbali nchini kote, wanapata huduma ya umeme.



Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya watoa huduma za fedha wakimsikiliza Kamishna wa Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Charles Mwamwaja (hayupo pichani), wakati wa mafunzo ya Sera, Sheria na Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha kwa wadau wa Kanda ya Kati kutoka mikoa ya Iringa Dodoma na Singida, yaliyofanyika mjini Morogoro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Taasisi za fedha kuwatambua wakulima

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, alibainisha kuwa katika kukabiliana na changamoto kadhaa zinazowakabili wakulima ikiwamo kutotambulika rasmi kwenye taasisi za kifedha, tayari serikali imeanza kutoa vitambulisho maalum kwa ajili yao vitakavyowatambulisha hususani wanapohitaji huduma za kifedha.

Hasunga alibainisha hayo kwenye mkutano mkuu wa wadau wa korosho uliofanyika mwishoni mwa wiki mkoani Lindi, ambao ulihudhuriwa na wadau kadhaa wakiwamo wakulima, wafanyabiashara wa pembejeo na wa zao hilo.

"Vitambulisho hivyo vya kisasa vitakuwa na 'chip' maalumu itakayobeba taarifa zote muhimu kuhusu mkulima hatua ambayo tunaamini itazirahisishia taasisi za fedha mlolongo mrefu wa kukusanya taarifa za wadau hao na hivyo kuwapatia mikopo kwa wakati," alisema Waziri Hasunga.

Aidha, katika mkutano huo alikabidhi vitambulisho hivyo vya mfano kwa wakulima 15 wa awali."Pia kwa sasa serikali tunatathmini upya sera ya masoko ikiwamo suala zima la kilimo cha mkataba ili wakulima wetu waweze kujua bei za bidhaa zao mapema kabisa," alibainisha Waziri Hasunga.

Wakati huo huo, wadau mbalimbali wa kilimo cha zao la korosho nchini wameonyesha kuvutiwa na huduma mpya ya NBC Shambani, huku wakibainisha ujio wa huduma hiyo maalumu kwa ajili ya wakulima utaondoa changamoto za muda mrefu ikiwamo kutopata mikopo kwa wakati sahihi.

Wakizungumza wakati walipotembelea banda la huduma za benki hiyo kwenye mkutano mkuu wa wadau wa korosho mkoani Lindi, baadhi ya wadau wa zao hilo walisema miongoni mwa changamoto zinazowakabili ni kutopata mikopo kwa wakati sahihi, hivyo wanaamini ujio wa huduma hiyo mpya utaondoa changamoto hiyo.

"Licha ya uwapo wa huduma nyingi za kibenki kwa ajili ya wakulima bado tumeendelea kukabiliwa na changamoto kadhaa za huduma za kifedha ikiwamo ucheleweshwaji wa mikopo na tunapoipata inakuwa sio wakati sahihi, hivyo kusababisha wengi wetu kuitumia kwa matumizi yasiyokusudiwa.

"Ni matarajio yetu ujio wa huduma NBC Shambani utatatua changamoto hii na sisi tupo tayari kuipokea," alisema Salum Muhila, mkulima wa korosho kutoka wilaya ya Liwale, mkoani Lindi."

Awali, akifafanua kuhusu huduma hiyo kwa wadau hao, Mkuu wa Kitengo cha wateja Wadogo na wa Kati kutoka Benki ya NBC, Raymond Urassa, alisema inalenga wadau wote wanaojihusisha na mnyororo wa biashara ya kilimo wakiwamo wasambazaji wa pembejeo za kilimo, wakulima na wasafirishaji wa mazao ya kilimo na tayari imepoanza kutumiwa kwa wingi na wakulima wa zao la ufuta.

"Kwa kuwa NBC Shambani imekuja mahususi kwa ajili ya wadau wa kilimo tafsiri yake ni kwamba ufanisi wake upo kwenye kutatua changamoto hasa zinazowagusa wadau hao ikiwamo kupata mikopo kwa wakati sahihi ili mkulima autumie mkopo huo kufanya kile hasa kinachotakiwa kufanywa kwa wakati huo," alisisitiza.

Alibainisha huduma hiyo inatoa fursa kwa wadau hao kuwa na akaunti ya vikundi vya wakulima kama vile AMCOS na vikundi vingine pamoja na akaunti ya mkulima mmoja mmoja.

# NEC yaombwa kutoa haki kwa vyama vyote

**Na Romana Mallya**

VIONGOZI wa dini wameishauri Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuwa ili kudumisha amani katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu, isitoe upendeleo kwa chama kimoja cha siasa.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam katika mkutano wa NEC na viongozi wa dini kuhusu uchaguzi huo.

Mkurugenzi wa Kurugenzi kutoka Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padri Florence Rutahiwa, alisema ombi lao kwa NEC ni kuhakikisha hawapendelei chama kilichoshika dola.

"Ukipendelea chama kimoja kilichoshika dola amani haitakuwapo, waliopewa dhamana wanatakiwa watusikilize sana viongozi wa dini maadili yafuatwe," alisema

Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum, alisema viongozi wa dini wana nafasi kubwa katika eneo la amani.

"Wananchi ni waumini wetu katika misikiti na makanisa, yaliyozungumzwa na Mwenyekiti wa Tume tunapaswa kuyachukua na kuwaeleza waumini namna bora ya kushiriki Uchaguzi Mkuu kwa kufuata nidhamu na taratibu," alisema.

Mchungaji wa Kanisa la Moravian Tanzania Jimbo la Mashariki, Neema Kashiririka, alisema ni vizuri viongozi wa dini wawaelekeze waumini umuhimu wa amani kwa sababu inapokuwapo watachagua kiongozi mzuri.

Awali Mwenyekiti wa Tume, Jaji mstaafu, Semistocles Kaijage, aliwaomba viongozi wa dini kuhubiri amani na kuwasisitizia wagombea wa vyama vya siasa kuheshimu, kutii na kuzingatia sheria za nchi na kanuni za tume katika uchaguzi mkuu.

Alisema wanatarajia ndani ya wiki hii kukutana na wadau kujadili nafasi zao kama viongozi katika kufanikisha uchaguzi.

"Tutasimamia uchaguzi kwa kuzingatia katiba, sheria na kanuni ili uwe huru, wa wazi na haki, wakuaminika na kuweka ushindani wa vyama vyote vinavyoshiriki," alisema.

Aliwaomba viongozi wa dini kuhimiza kampeni zitakazofanyika ziwe za kistaarabu na zenye kuepuka vitendo vya uvunjifu wa amani ya nchi.

Naye, Mkurugenzi wa Uchaguzi NEC, Dk. Wilson Mahera, alisema wanatarajia viongozi wa dini watatumia nyumba za ibada kuhamasisha waumini kuweka maslahi ya Taifa kwanza na ushabiki wa vyama vya siasa baadaye.

Alisema kuanzia Agosti 5 hadi Agosti 15 Tume ilitoa fomu za uteuzi kwa wagombea wa kiti cha urais, makamu wa rais kutoka vyama vya siasa 16 kati ya 19 vyenye usajili wa kudumu.

Nipashe
# TESA
Jumanne Agosti 18, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

**Wanasayansi wafafanua miti inavyofahamiana, kuwasiliana**



Ukurasa 14

Ndivyo sheria ilivyokuwa muhimili kazi zenye staha



Ukurasa 13

**Ilipo nafasi yako Mtanzania serikali inaponadi mafanikio**

ELIMU

## NA SABATO KASIKA

# Wilaya iliyokuwa mkiani kielimu ilivyoibukia kileleni

KILICHOFANYIKA wilayani Ruangwa mkoani Lindi, unaweza kusema si kazi nyepesi kwani kwa miaka tisa ilikuwa ikiburuza mkia au ikijikongoja kwa kushika nafasi ya pili kutoka mwisho katika matokeo ya mitihani, imechomoza na sasa inaongoza kiwilaya.

Ilikuwa inaburuza mkoa kwenye matokeo ya kidato cha nne kati ya wilaya sita za mkoa huo lakini leo ni tofauti. Kumekuwapo na mabadiliko makubwa tangu mwaka 2016 hadi sasa kufuatia jitihada za dhati na za pamoja za kuboresha elimu na leo wilaya hiyo inashika nafasi ya tatu kwa ufaulu.

Mojawapo ya hatua hizo ni kila mdau wa elimu kutimiza wajibu wake, huku serikali akiruhusu asasi za kiraia kubuni na kuratibu mradi wa kimkakati wa kuhamasisha maboresho ya elimu ya sekondari katika wilaya hiyo.

Hivyo ndivyo anavyosema, Ofisa Elimu Sekondari Wilaya ya Ruangwa, Ernest Haule, kuwa ujio wa mradi wa kuhamasisha maboresho ya elimu, umechangia kufanikisha jitihada za serikali kuboresha elimu. Moja kati ya sababu iliyokuwa ikitajwa kuchangia uduni wa elimu wilayani humo ni jamii kukosa msukumo wa kuwekeza katika elimu, hali ambayo iliirudisha nyuma.

Wahusika wanaotajwa hapa ni wanafunzi ambao ndiyo walengwa wakuu, wazazi, walezi, bodi za shule za sekondari, walimu na idara ya elimu ya Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mnacho wilayani Ruangwa, katika moja ya ziara zake za kikazi. **PICHA: MTANDAO**

### MATOKEO MAKUBWA SASA

Haule anasema, mwaka 2018 na 2019 Ruangwa ilishika nafasi ya kwanza kidato cha sita kwa kufaulisha asilimia 100 ikifuatiwa na Wilaya ya Liwale kwa asilimia 98, huku Nachingwea ikiwa na asilimia 94.

"Hiyo ni kati ya wilaya sita za mkoa wa Lindi, na kwa kidato cha nne mwaka 2018, tulifaulisha kwa asilimia 64 na kushika nafasi ya tano, huku mwaka 2019 tukifikia ufaulu wa asilimia 79 na kushika nafasi ya tatu kimkoa," anasema Haule.

Ofisa elimu huyo anaongeza kuwa kwa sasa lengo lao ni kupunguza sifuri kidato cha nne kwa kuongeza alama za ufaulu ili ifikapo mwaka 2025 washike nafasi ya kwanza kimkoa na wawe bora kitaifa.

"Ninasema hivyo kwa sababu, tulipata sifuri 68, lakini mwaka uliofuata wa 2019 zikapungua na kuwa 32, kwa hiyo hii inaonyesha kwamba, japo hatujazimaliza tunakwenda vizuri na tutatimiza malengo tuliojiwekea," anaahidi.

Anasema, kwa sasa wanafunzi wanatimiza wajibu wao wa kuhudhuria masomo, huku wazazi na walezi nao wakiwahimiza kusoma kwa bidii, kwa kuwa wanatambua umuhimu wa elimu.

### JITIHADA ZILIZOFANYWA

Haule anasema, kuna asasi za kiraia zenye mchango mkubwa katika kuboresha elimu Ruangwa ambazo zimeshirikishwa. Anaitaja Asasi ya Kuunganisha Vijana Kimaendeleo Ruangwa (AKUVIKIRU), ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikifanya kazi wilayani hapo.

Aeleza kuwa inashirikiana na serikali kwa karibu na imebuni na kuratibu mradi wa kimkakati wa kuhamasisha maboresho ya elimu ya sekondari wilayani Ruangwa.

"Kwa kiasi kikubwa imesaidia kuboresha elimu wilayani mwetu, kwani mradi wa kuhamasisha maboresho ya elimu ya sekondari umesaidia kufikia mafanikio haya na kuongeza uwajibikaji," anasema.

Anasema, wananchi kwa sasa wana uwezo wa kuhoji matumizi ya fedha zao zinazoelekezwa kwenye miradi shuleni, bila woga kama ilivyokuwa miaka ya nyuma kabla ya mradi huo.

"Kadhalika, shule za Narungombe, Ruangwa, Kassim Majaliwa, Hawa Mchopa, Nkowe na Mbekenyera zina mabweni kati ya mawili hadi manne kila moja na mabwalo ya chakula," anasema.

Mbali na kufikia hatua hiyo, anasema, kuna ongezeko la shule kutoka 12 miaka mitano iliyopita hadi kufikia 20 sasa, pia wamejenga nyumba za walimu wastani wa tatu kila shule.

"Vilevile tumeongeza madarasa kutoka 96 hadi kufikia 152, na tumepandisha hadhi sekondari tatu kuwa za kidato cha sita, na kwamba kufikia mwishoni mwa mwaka huu zitakuwa tano.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Rashidi Namkulala, anasema, mradi huo umejibu maswali mengi yaliyokosa majibu ikiwamo wananchi kujitoa kusaidia miradi ya ujenzi wa shule na kuchangia fedha au chakula ili watoto wawe na uhakika wa kusoma.

### ILIVYOANZA KAZI

Mratibu wa mradi wa AKUVIKIRU, Simon Ndallu, anasema, kufanya utafiti kwa zaidi ya miezi 18, hatimaye mradi huo ulianza rasmi mwaka 2017 na umezifikia kata 12 kati ya 22 za wilaya hiyo.

"Mradi umepata mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na kuhamasisha wananchi kujenga sekondari katika kata tatu za Matambarale, Chibula na Mandarawe," anasema Ndallu.

Ndallu anasema, asasi inahamasisha wananchi kila kijiji kwa ajili ya kujitolea na kuchangia fedha kutoka katika mazao ya biashara, ambazo zimetumika kujenga sekondari katika kata hizo.

"Kati ya shule hizo mbili za Chibula na Matambarale, wameanza kupokea wanafunzi mwaka huu, huku ya Mandarawe ikitarajiwa kuanza rasmi mwakani 2021," anasema.

Anasema, kabla ya wananchi kujitoa na kuchangia ujenzi wa shule hizo, AKUVIKIRU ilifanya mikutano ya hamasa na ushawishi zaidi ya mwaka mmoja katika vijiji 39 vya kata 12 za mradi.

INAENDELEA UK.12

SAYANSI

**NA MICHAEL ENEZA**

# Wanasayansi wafafanua miti inavyofahamiana, kuwasiliana



Misitu na mimea mingine inaelezwa huwasiliana hadi kuunda urafiki. **PICHA: MTANDAO**

KUNA usemi kuwa ukistaajabu ya Musa, utaona ya Firauni, hivyo wakati watu wameshangaa mambo mengi kuhusu wanyama na wadudu, ukifuatilia wanasayansi wanachosema kuhusu miti, unaweza kuchanganyikiwa.

Ni miaka miwili sasa hoja inaendelea kujadiliwa iwapo miti inaunda urafiki na mingine inakumbuka yaliyopita. Ni dhana ambayo inaongeza ufahamu zaidi kuwa miti inaelewa ishara na hata sauti, wakati fulani kukiwa na taarifa kuwa mwanamfalme wa Uingereza, Prince Charles, huongea na miti.

Maelezo hayo yalianza kusambazwa baada ya mwanasayansi na mtunza misitu nchini Ujerumani kuandika kitabu, 'Maisha Yaliyojificha ya Miti,' akiwa ametumia miongo kadhaa katika fani hiyo ya kuichunguza, kuikagua na kuihudumia.

Moja ya maeneo ya fani yake na ufahamu wa miti unampa sifa kama ya Prince Charles kuwa ananong'oneza mti na anaweza kujua kama ishara hiyo imeeleweka.

Hadi miaka miwili iliyopita alikuwa ameandika vitabu vitatu katika eneo hilo, vingine vikiwa ni 'Miti msituni ni jamii,' 'miti inaweza kufungamana kama wanandoa wazee na kusaidiana.'

> Gwaride la siafu katika kusimamia wadudu kazi kutafuta na kupitisha chakula kwenda kwa malkia lina mistari iliyonyooka kuliko kwata ya jeshi.

Amefanya mahojiano mara kadhaa na majarida ya kitaaluma ambayo mhakiki anayafanyia mapitio na kutoa maoni yake.

Kilichomshangaza zaidi mhakiki huyo ni jinsi mtaalamu huyo anavyozungumzia miti kuwa na kumbukumbu, akieleza kisa cha kuwapo kwa ukame wakati fulani na nyakati zilizofuata, miti ambayo ilipata tatizo kubwa zaidi wakati wa ukame ilikuwa inatumia maji kidogo zaidi kuliko mingine wakati wa mvua na kiangazi chepesi.

Ni kwa sababu ilijifunza kuwa wakati wa kiangazi kikali au ukame kuna shida ya maji hivyo iyatunze yatumike wakati kiangazi kikali kikirudi. Ina maana miti inafanya uamuzi na huamua mambo na pia kujifunza na kukumbuka mengine, mfano kujua kuwa ukame unaweza kurudi hivyo, kutunza maji yaliyopo ili yasimalizike.

Baadhi ya wanasayansi walianza kumshambulia mtaalamu huyo, Peter Wohlleben, kuwa anajadili miti kana kwamba anazungumzia wanadamu na kwamba anatafuta namna ya kufikia tamati au mwelekeo kuwa miti ina vipaji kama watu.

Wohlleben, anajibu kuwa anafanya hivyo kwa makusudi, siyo kwa kupotosha ila kuonyesha au kudhihirisha yale ayayoona akiwa katikati ya miti na kukagua kinachotokea, au ukitaja hilo kibinadamu utasema 'kile miti inachotenda.' Mhakiki huyo ambaye amefanya ufuatiliaji wa masuala hayo kitaalamu anatoa mifano kadhaa, mmoja ni miti ambayo kwa kawaida matawi yake yanasambaa pande zote kutoka mtu iliposimama, lakini miti hiyo ikiwa rafiki, matawi yataelekezwa upande mwingine.

Anasema kuwa ameona hali hiyo ikitokea mara moja katika 50 kwa wastani, ambako urafiki maalum unaonekana kati ya miti.

Ina maana katika ushindani wa kupata mwanga juu ya ardhi na kupata maji na chumvichumvi chini ya ardhi, miti inatofautisha kati ya mmoja na mwingine.

Isitoshe, anasema kuwa hulka kwa mfano ya kuelekeza matawi upande mwingine na siyo kule mti rafiki ulipo inajulikana sana kwa watunza misitu kuwa sio ugunduzi mpya uliotokea hivi karibuni.

Anaeleza kuwa katika hali hiyo, mtu anakuwa mwangalifu kuhusu kukata mti ambao una mti rafiki kando, kwani huo mwingine utakufa pia kama mmoja utakatwa.

Ni kama ilivyo kwa wanandoa wa siku nyingi akifa mmoja, wa pili hakai au anaishi muda mfupi.

Akijaribu kueleza jinsi hali hiyo inavyotokea au jinsi ilivyojengeka katika mimea, mhakiki anasema miti ina aina ya mawasiliano ya kikemikali na viishara vya umeme ambavyo kwa jumla vinakuwa ni kama lugha inayozungumzwa.

Unaweza kuona kuwa ni hatua ya jinsi mawasiliano yanavyojengwa katika maisha ya viumbe, kutoka mawimbi ya kemikali na umeme kwa mimea, hadi sauti za aina tofauti za wadudu na milio ya aina mbalimbali kwa wanyama, hadi uwezo wa kuzungumza ambao ni wa binadamu peke yake miongoni mwa viumbe hai.

Kinachoashiriwa hapo ni kuwa miti si kama mashine za roboti zinazokua na jua, maji.

Mtaalamu huyo anakwenda mbali zaidi kuanza kuhoji mpangilio mzima wa jinsi binadamu kwa kawaida anavyoiona mimea na hasa miti, halafu aunde ngazi ya ubora wa viumbe kuanzia miti isiyo na akili hadi wadudu, wanyama na kufikia binadamu.

Tatizo la ubora wa viumbe kwa viwango vya uwepo wa akili na lugha limekuwepo kwa karne nyingi, kwa mfano inajulikana muda wote kuwa nyuki wanaunda mifumo ya vyumba na uwiano wa hewa na kudhibiti joto katika maskani za kutengeneza asali ambayo imechukua binadamu muda kuelewa mantiki ya mifumo hiyo.

Gwaride la siafu katika kusimamia wadudu kazi kutafuta na kupitisha chakula kwenda kwa malkia lina mistari iliyonyooka kuliko kwata ya jeshi.

## Wilaya iliyokuwa mkiani kielimu ilivyoibukia kileleni

**INATOKA UK.11**

Anasema, mbali na mikutano ya hadhara, mradi pia uliwaleta pamoja wajumbe wa bodi za shule zote na kuwajengea uwezo ili watambue majukumu yao.

"Kabla ya mradi, baadhi ya wajumbe walikuwa hawajui wajibu wao, lakini sasa wanajua na ndiyo maana shule zimeanza kuboreshwa na kutoa matokeo chanya," anasema.

Kwa upande wake Msimamizi Mkuu wa Mradi wa asasi hiyo, Abdul Mitumba, anasema, wakati wote wa mradi, wamekuwa wakitoa mafunzo kwa wajumbe wa kamati za ufuatiliaji wa rasilimali za umma ngazi ya wilaya ya Ruangwa (PETS), ili kuhakikisha fedha na mali nyingine zinazoelekezwa katika shule hizo zinatumika vizuri.

Anafafanua kuwa kabla ya mradi kuanza, wazazi na walezi kazi yao ilikuwa ni kuwaandikisha watoto shule, lakini hawakufuatilia maendeleo yao shuleni, hali iliyokwamisha uwajibikaji.

"Walimu nao waliona kazi yao ni kufundisha tu, hawakuwa wakifanya jitihada zozote kuhakikisha wanafunzi wanafika shule kwa wakati, lakini sasa wanawasiliana na wazazi kila wakati kuhakikisha wanafunzi wanafika shule kila siku ya masomo," anasema.

### MBUNGE AWATIA MOYO

Mbunge wa Ruangwa ambaye pia ni Waziri Mkuu wa Tanzania, Kassim Majaliwa anawataka viongozi wa asasi hiyo wasichoke, waendelee kufanya kazi hiyo ili kuikwamua jamii kutoka katika ujinga na umaskini.

"Niwapongeze AKUVIKIRU kwa kazi mnazofanya katika mradi huu, mmekuwa mfano wa kuigwa wilayani Ruangwa, endeleeni msichoke kufanya kazi hii," waziri mkuu anasema.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Ilipo nafasi yako Mtanzania serikali inaponadi mafanikio

JUHUDI za kuwavusha Watanzania kwenye umaskini na kuinua maisha yao ndicho kinachoendelea katika mchakato wa kuelekea kwenye uchaguzi mkuu, kampeni zikitaja mafanikio na kulenga mambo makubwa ya kuwafanya wapigakura kuwachagua tena.

La msingi ni wananchi kujitambua na kujua kuwa maendeleo ni jukumu lao na si kudhani kuwa ni suala la serikali au chama tawala au wanasiasa wanaoomba ridhaa ya kupewa kazi ya uwakilishi uwe wa kupitia majimbo au utaratibu mwingine.

Kama kuna mambo mema yamefanywa na serikali ni yao na wanajibika kuyalinda na kuyasimamia na kulidumisha mafanikio ili yawe endelevu na kuzungumzia wanapoona yanatetereka.

Kila wakati watu wakitazama mafanikio kuanzia awamu zilizotangulia mfano ya nne na jinsi kila mmoja anavyoweza kusema taifa linasonga mbele hivyo waone wanao wajibu wa kulinda wa kumiliki mafanikio hayo na kuyalinda.

Mathalani, wakati akiondoka madarakani Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda, alizungumzia mafanikio ya awamu ya nne akitaja mambo mengi, pengine la mojawapo ni elimu.

"Mwaka 2005 awamu hii ikiingia madarakani shule za msingi zilikuwa 14,257 na leo inapoondoka zipo 16,538."

Anasema zaidi kuwa, wakati wanafunzi wa shule za msingi waliongezeka kutoka 7,541,208 hadi 8,202,892 katika kipindi hicho. Elimu ya sekondari nayo ilishamiri sekondari mwaka 2015 zilifikia 4,753 wakati mwaka 2005 zilikuwa 1,745, kwa mujibu wa mstaafu Pinda.

Akizungumzia wanafunzi alikumbusha kuwa kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita idadi ilikuwa ndogo kiasi cha 524,325 serikali ilipoingia madarakani lakini wakati inaondoka 2015 walifikia milioni 1.7.

Si hivyo tu, alisema vyuo vikuu vilikuwa 23 mwaka 2005 lakini viliongezeka hadi 49 na wanafunzi waliodahiliwa kwa takwimu za mwaka 2013/14 walikuwa zaidi 204,176, ikilinganishwa na 40,000 waliodahiliwa kabla ya awamu ya nne.

Tanzania imepata mafanikio mengine mengi kwa namba na ubora kuanzia afya ongezeko la hospitali, ubora wa huduma, kuongeza umri wa kuishi, barabara, kilimo, mawasiliano, usambazaji umeme na maji vijijini, ufugaji na kwa ujumla sekta zote ikiwa pia na siasa kwa vile Watanzania wanaongeza ushindani kwenye masuala ya kidemokrasia.

Kwa miaka mitano awamu ya tano ina mengi ya kujivunia kwa kuwa kila kitu kimepaa na kuifanya Tanzania kuingia kwenye uchumi wa kati. Lakini iwe miundombinu ya umeme, maji, madarasa na madaraja lazima umma ujue kuwa unawajibika kulinda na kutunza ili mafanikio yadumu.



Ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) unaoendelea kukamilika jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

### AWAMU YA TANO

Mathalani, kuanzia Januari 2016, idadi kubwa ya wanafunzi wanaoandikishwa darasa la kwanza na wanaojiunga na kidato cha kwanza kwa shule za umma imeongezeka zaidi kutokana na utekelezaji wa sera ya serikali kugharamia elimu.

Waziri wa Nchi,Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali zaMitaa(TAMISEMI) Selemani Jafo, anasema, idadi ya walioandikishwa imeongezeka kutoka 10,201,972 mwaka 2015 hadi 12,034,599 mwaka 2020, kwa shule za msingi.

Aidha, kwa upande wa sekondari anasema idadi ya wanafunzi wakati wanaingia madarakani ilifikia milioni 1.8 mwaka 2016 lakini leo wamefikia milioni 2.02 na kwamba tangu kuanza kwa utekelezaji wa kugharamia elimu serikali kuanzia Desemba 2015 hadi Juni, 2020 imetumia Sh. trilioni 1.09 kugharamia elimu bila malipo.

Aidha, hadi kufikia Juni, mwaka huu ujenzi wa shule mpya za msingi 905 ulikuwa umekamilika hivyo kuongeza idadi yake kutoka 16,899 mwaka 2015 hadi 17,804 mwaka 2020.

Sekondari mpya 228 zimejengwa na hivyo kuongezeka kutoka shule 4,708 mwaka 2016 hadi 5,330 mwaka 2020. Pamoja na ujenzi huo shule kongwe zimekarabatiwa na kuwekewa miundombinu mipya ili kuboresha elimu.

Mafanikio hayo yatadumu iwapo shule zilizojengwa na kuboreshwa zitalindwa, wazazi na walezi kupeleka watoto shule, kufuatilia na kujua maendeleo ya watoto wao shuleni na kushirikiana na serikali kwenye miradi ya kuboresha elimu kwa kujitolea.

Serikali imefanya juhudi nyingi, shule zipo na zinaendelea kujengwa ni jukumu la jamii na wanafunzi kulinda maendeleo ya elimu kutunza madawati ili kukomesha watoto kukaa chini. Ni budi shule ziendeshwe kwa ujasiriamali ziwe na vyoo, vitabu, mabweni ili kulinda na kuendeleza mafanikio. Utafiti ufanyike na mapendekezo yatolewe ya jinsi ya kulinda mafanikio hayo.

### KUDHIBITI MIMBA

Maendeleo wananchi wanayoyaona ni mtaji lakini ili elimu iwe na tija ni lazima kuondoa na kukabiliana na vyanzo vya mabinti kupata mimba na kushindwa kusoma.

Ni muhimu kujenga mabweni ili kudhibiti mabinti kutembea umbali mrefu kwenda shuleni. Aidha, kuwawekea mazingira na huduma muhimu kama maji, chakula na mahitaji maalum kama tauli za wanawake ili kuepusha uwezekano wa kukosa masomo kwa sababu ambazo zingeweza kuzuilika.

Jamii ihamasishwe kuacha unyanyasaji wa mabinti kingono, aidha sheria zitumike kuadhibu wanaowapa watoto mimba na sheria za kuoza watoto zifutwe wakati na mila na desturi potofu za kuoza watoto zikipigwa marufuku.

> Raia wana wajibu wa kuachana na mienendo ya kushauwishi kupewa rushwa, au kupendelea kutoa rushwa au kurudisha nyuma juhudi hizo kwa kuendeleza uzembe na kuacha uwajibikaji.

### KUDHIBITI RUSHWA

Serikali imekomesha rushwa na imeidhibiti ili kuhakikisha kuwa utoaji elimu, utendaji ofisini, huduma za jamii na masuala mengi yanayowahusu wananchi yanaimarika. Kwa ujumla kila huduma inayotolewa na serikali ameimarishwa na kumuongezea Mtanzania furaha.

Kelele za hakuna uwajibikaji kwa watumishi wa umma, kuwalaumu kuwa wamezidi utoro, hawakai ofisini badala yake wanazungukia semina, warsha na makongamano, kuanzia wakuu wa wilaya, wakurugenzi na watendaji karibu wote zimekoma.

Raia wana wajibu wa kuachana na mienendo ya kushauwishi kupewa rushwa, au kupendelea kutoa rushwa au kurudisha nyuma juhudi hizo kwa kuendeleza uzembe na kuacha uwajibikaji.

### KUPUNGUA URASIMU

Suala la urasimu lililokuwa donda ndugu na kujitokeza zaidi kwa wananchi kuambiwa 'njoo kesho,' 'tupo kwenye mchakato' suala lako linafanyiwa kazi' limekomeshwa na awamu ya tano.

Watanzania wana wajibu wa kufuatilia na kuhakikisha kuwa mambo hayo hayarudi tena kwenye jamii ili kulinda mafanikio na maendeleo.

### MIGOGORO ARDHI

Migogoro ya wawekezaji na wananchi, matatizo ya ardhi yaliyokuwa yanadaiwa kuongezeka na wengine wakilalamikia wenye haki kukandamizwa na wenye hela kubebwa na viongozi wa serikali imefikia ukingoni.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Ndivyo sheria ilivyokuwa muhimili kazi zenye staha



Ofisa Habari wa ATE , Yunga Kanuda, akizungumza kwenye mkutano wa vijana wa ajira zenye staha hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

NURU ni mstaafu si kwa uzee bali kilichomuondoa kazini ni vidonda vilivyotokana na kuumizwa na tindikali inayotumiwa kwenye kuzalisha nguo.

Akiwa na miaka 37 mama huyo mwenye watoto watano analazimika kuacha kazi kutokana na tindikali inayotumiwa kwenye kiwanda cha nguo kuchimba viganja vya mikono yake na kumsababishia vidondo visivyopona hivyo mwajiri wake kumuondoa kazini kupisha wengine wenye afya.

Nuru alikuwa akifanyakazi kwa mkataba wa mwaka mmoja na alikuwa anakata majora ya kanga na vitenge kwenye kiwanda kimoja cha nguo jijini Dar es Salaam.

Kabla ya kuondoka kazini mwaka 2017 pamoja wanawake wengine wanaokata majora kwa kutumia mikasa lakini hawana glovu za kuzuia tindikali isiwaumize hata walipokuwa wakilalamika mwajiri aliwaambia anayeona hawezi aondoke . Wanasema hata hivyo huo ndiyo utaratibu wa kiwanda hicho, huwatumikisha bila vitendea kazi wala vifaa kinga na pale vidonda vitakapozidi wanaondolewa lakini mwajiri husubiri mkataba unapofika ukingoni.

Wafanyakazi hao huondoka bila fidia wala matibabu na wengi huishia kuugusa vidonda kwa gharama kubwa. Lakini wanapona baada ya kuacha kushika tindikali hiyo.

> "Anashauri wote walipwe kulingana na kiwango cha elimu kama ni shahada, cheti au astashada badala ya kupendelea baadhi ya fani.

Nuru ni miongoni mwa wafanyakazi wengi wanaoteseka kutokana na ukosefu wa kazi unaowalazimisha wengi kufanyakazi zisizo na staha hasa kwenye sekta binafsi na walio katika ajira zisizo rasmi.

Kazi zisizo na staha zinawalazimisha wasichana kunyanyaswa kingono na waajiri au wakuu wa vitengo ili kupandishwa daraja na kuongezewa mshahara au kupata mkataba hasa kwa vibarua.

Aidha, zinawatumbukiza kwenye udhalilishaji kama kulazimishwa kuvaa mavazi mafupi, kuonyesha maungo ili kuvutia wateja. Ni kwa wanaofanyakazi kwenye baa, hotelini au kwenye nyumba za wageni.

Waendesha pikipiki nao hawako salama ajira zao si rasmi. Japo wana mkataba wa kumpelekea bosi Sh. 70,000 kila wiki wanalazimika kuendesha boda bila kofia ngumu pikipiki ikipotea au kuporwa ndiyo wanaoilipa na endapo wataumia wajiri huwatelekeza.

Hayo na mengine mengi ni miongoni mwa mengi yanayojadiliwa katika mkutano wa vijana kuhusu umuhimu wa kazi zenye staha na mbinu za kukabiliana na changamoto zinazoletwa na kazi zisiho na heshima au staha.

Maridadi Phanuel ni ofisa wa programu ya masuala ya uongozi kutoka Shirika la Kazi Duniani (ILO), akizungumzia changamoto zinazowapata wafanyakazi anasema ni matokeo ya waajiri kukosa urafiki na waajiriwa.

Anaeleza kuwa ili uzalishai uwe wa tija ni lazima kuwathamani ili wawe na morali, wazalishe zaidi na kuongeza tija lakini pale wanapodharauliwa uzalishaji unapoporomoka.

"Ili kufanikisha mpango wa ajira zenye staha waajiri wanapaswa kuandaa na kutekeleza mikakati, sera na sheria za ndani ya mashirika au kampuni zao yanayolinda maslahi ya wafanyakazi kulingana na sheria, sera na taratibu za kazi za kitaifa na za kimataifa."

Anasema mahali pa kazi ni lazima kufuata sheria, kwa mfano Tanzania inaongozwa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004.

Aidha, Phanuel anasema , kuwapa wafanyakazi stahili zao mojawapo ni kuwaandalia mikataba ya kazi ya kisheria, kulipa mishahara kwa wakati, kuwapa vitendea kazi na vifaa kinga, kutoa likizo ya kazi, uzazi, kuwasilisha michango kwenye mifuko ya jamii , kuruhusu vyama vya wafanyakazi na kuendeleza majadiliano ya utatu kunapoibuka changamoto.

"Utatu unahusisha vyama vya wafanyakazi, waajiri, wadau wengine pamoja na serikali ili kupata ufumbuzi wa changamoto kazini," anasema.

Katika mkutano huo unaoratibiwa na shirika la ActionAid, wadau mbalimbali wakiwamo Shirika la ILO, Chama cha Waajiri (ATE), Jumuiya ya Waajiri Zanzibar (ZANEMA) Chama cha Wafanyakazi wa Viwandani, Taasisi za Biashara, Elimu na Huduma (TUICO), waganga wa wilaya , wanasheria , maofisa kazi, wafanyakazi kutoka sekta mbalimbali kama wanaeleza kwa kauli moja kuwa suala la ajira zenye staha ni muhimu.

Hata hivyo, mkutano huo uliukosoa utitiri wa vyama vya wafanyakazi nchini uliodaiwa una maslahi 'binafsi' ambayo pengine si kusaidia wanachama wao.

Kwa upande mwingine wafanyakazi wanazungumzia ubaguzi kijinsia kazini unaowalipa wanaume mishahara na posho zaidi kuliko wanawake hata kama kinamama wana ujuzi zaidi.

Asha Khamisi kutoka Jumuiya ya Wauguzi Zanzibar anahoji kwanini serikali inalipa watumishi wake kwa kuangalia taaluma badala ya kiwango cha elimu.

Anasema madaktari hulipwa kuliko wauguzi , lakini pia kuna kada kama za sayansi zenye mishahara mikubwa ikilinganishwa na nyingine za sanaa (arts) jambo linasababisha malalamiko miongoni mwa watumishi.

Anashauri wote walipwe kulingana na kiwango cha elimu kama ni shahada, cheti au astashada badala ya kupendelea baadhi ya fani.

Jovina Nawenzake, Ofisa Mkuu wa Programu na Sera wa ActionAid, anasema utafiti uliofanyika hivi karibuni unaonyesha ongezeko la ajira nchini lakini pamoja na ongezeko hilo kazi hizo nyingi hazina staha.

Anaeleza kuwa ili kazi ziwe na staha ni wakati wa maofisa ukaguzi wa kazi kufanya ukaguzi wa mara kwa mara sehemu za kazi ili kubaini mafanikio na changamoto na kuzifanyia kazi na hasa kusimamia staha kazini.

Anaamini kuwa ukaguzi wa mara kwa mara na kuzungumza na wafanyakazi utalazimisha waajiri kufuata sheria, kuondoa udhalilishaji, kuweka usawa wa kijinsi na kupatikana vitendea kazi pamoja na kuwasilisha michango ya mifuko ya jamii.

Aidha, anavikumbusha vyama wafanyakazi kama CWT cha walimu na TUICO kuwaelimisha wanachama wao kuhusu sera na sheria za kazi za kitaifa na kimataifa kuzisimamia na kudai haki zao kwa mujibu wa sheria.



# Watumishi Bunge wajiunga na JKT

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) limefungua mafunzo ya Operesheni Uchumi wa Kati mwaka 2020, kwa watumishi wa bunge, huku likiwataka kuwa wazalendo kwa nchi yao.

Akifungua mafunzo hayo jana katika Kikosi cha JKT Makutupora, Mwakilishi wa Mkuu wa JKT, Brigedia Jenerali Rajab Mabele, alisema yanalenga kuwatengeneza kuwa waaminifu kwa taifa lao na kuwataka kuzingatia makatazo yote waliyopewa.

Mabele ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi hilo (SUMA JKT), alisema kupitia mafunzo hayo, wanajengwa kuwa na nidhamu, ukakamavu, uzalendo na kupenda kazi.

Aliwataka baada ya kuhitimu mafunzo hayo kuwa waaminifu, watii na watumishi bora wenye uzalendo.

"Mtambue kuwa kila kitakachofanyika ni sehemu ya mafunzo na hakuna manyanyaso yoyote mtakayopewa. Zingatieni makatazo msipozingatia mafunzo yatakuwa magumu kwenu na sisi sio nia yetu tunataka mkawe bora, wakakamavu na uzalendo wa hali ya juu," alisema.

Naye Mkuu wa Utawala wa JKT, Kanali Julius Kadawi, alisema taasisi mbalimbali zimekuwa zikiomba mafunzo hayo kwa watumishi wake ili kuwa na uzalendo.

"Hadi sasa Wizara ya Mambo ya Nje (na Ushirikiano wa Afrika Mashariki) awamu tatu za watumishi zimepata mafunzo na sasa ni Bunge wamekuja watumishi 41. Nitoe rai kwa taasisi zingine ambazo watumishi wake hawajapita JKT waje kuwaombea mafunzo haya," alisema.

Awali, Mkuu wa Tawi la Mafunzo na Operesheni, Kanali Aisha Matanza, alisema mafunzo yatafanyika kwa wiki nne kwa watumishi hao na kuwataka kuyatumia vizuri katika utendaji kazi wao wa kila siku pindi warudipo kazini.

Alitaja mambo watakayofundishwa ni pamoja na utunzaji na utumiaji wa silaha ndogo, kwata, mbinu za kivita, ujanja wa porini, utimamu wa akili, uraia na uzalendo, usomaji wa ramani, usalama na utambuzi na kuchimba mahandaki.

**Mtambue kuwa kila kitakachofanyika ni sehemu ya mafunzo na hakuna manyanyaso yoyote mtakayopewa. Zingatieni makatazo msipozingatia mafunzo yatakuwa magumu kwenu na sisi sio nia yetu tunataka mkawe bora, wakakamavu na uzalendo wa hali ya juu.**

# Jaji Mkuu awataka majaji kusoma sheria za uchaguzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, amewataka majaji na mahakimu kusoma sheria na kanuni zote za uchaguzi mkuu, ili kutoa uamuzi wa mashauri ya uchaguzi kwa weledi na kutenda haki.

Prof. Juma aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua mafunzo ya namna bora ya uendeshaji wa mashauri ya uchaguzi kwa maofisa wa mahakama wapatao 282.

Alisema majaji pamoja na wote watakopata nafasi ya kusikiliza mashauri ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu, wanatakiwa kuwa na uelewa mpana juu ya sheria na kanuni zitakazotumika ili kutenda haki.

Pia alisema maofisa wote wa mahakama ambao watapata nafasi ya kusikiliza mashauri ya uchaguzi mwaka huu, wanatakiwa kutumia muda wao sasa kuzisoma sheria na kanuni ili kujiongezea uelewa.

"Tunatakiwa kutenda haki kwa mashauri yote yatakayoletwa kwetu na kuyafanyia kazi ili kutoa uamuzi kwa weledi na kuzingatia haki kwa wale watakaoonewa katika mchakato wa uchaguzi mkuu mwaka huu," alisema Jaji Mkuu.

**Duru ya kwanza ya mafunzo hayo inawahusisha waheshimiwa majaji wa Mahakama Kuu, Wasajili na Naibu Wasajili, Mahakimu Wakazi Wafawidhi wa Makahama za Hakimu Mkazi.**

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo maofisa wa mahakama kutoa uamuzi kwa weledi na haki kwa wakati.

"Mahakama isionekane kupendelea upande fulani wa uchaguzi bali iisaidie Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kuwapatia wananchi uchaguzi huru na wa haki. Pia majaji wajikite katika kusoma vifungu ambavyo vitawasaidia kutoa uamuzi wa mashauri ya uchaguzi kwa wakati," alisema.

Jaji Mkuu pia aliwataka maofisa wa mahakama kushughulikia mashauri ya jinai wakati wa kamapeni katika uchaguzi mkuu.

"Makosa ya jinai ambayo mnatakiwa kuyashugulikia ni yale ya wakati wa kampeni pamoja na wakati wa kupiga kura. Makosa hayo ni kama vile kujiandikisha maeneo zaidi ya moja, kupiga kura katika kituo zaidi ya kimoja, kudanganya kitambulisho na mengine mengi," alibainisha.

Sambamba na hilo, aliwataka majaji na mahakimu kuhakikisha hukumu za kesi wanazozitoa zinaandikwa kwa lugha nyepesi ili wananchi wazielewe.

Naye Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dk. Elieza Feleshi, alisema mafunzo hayo yameandaliwa na Mahakama ya Tanzania kwa kushirikiana na Chuo cha Uongozi wa Mahakama (IJA) kilichoko Lushoto mkoani Tanga.

Jaji Feleshi alisema mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo maofisa wa mahakama na kuwaandaa kutoa haki kwenye mashauri ya uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani.

"Duru ya kwanza ya mafunzo hayo inawahusisha waheshimiwa majaji wa Mahakama Kuu, Wasajili na Naibu Wasajili, Mahakimu Wakazi Wafawidhi wa Makahama za Hakimu Mkazi," alisema.



Mkazi wa Kijiji cha Matumbulu, nje kidogo ya Jiji la Dodoma, Nowadia Mganga, akiponda kokoto ili kujipatia ujira wa siku kijijini hapo, wikiendi. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Askofu ataka wala rushwa 'wakatwe'

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KANISA la Biblia Tanzania limewataka Watanzania kutowachagua viongozi wanaotoa rushwa kwenye uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Askofu Mkuu wa Kanisa hilo, John Mchopa, alitoa rai hiyo juzi katika ibada ya kuwasimika viongozi wa Kanda ya Kati iliyofanyika jijini hapa.

Alisema wakichagua viongozi watoa rushwa watajinyima haki yao ya msingi kikatiba ya kuchagua viongozi bora wasiotokana na rushwa.

Mchopa alisema kitendo cha kutoa rushwa ya fedha na mali ni laana na chukizo mbele za Mungu.

"Watanzania mkiwachagua viongozi wa jinsi hii, mtajikuta mkikosa haki za kimsingi kutokana na gharama walizozitoa kwa ajili ya kutaka uongozi kutoka kwenu," alisema.

"Tanzania inawataka viongozi wenye hofu ya Mungu na watakaowatumikia Watanzania bila kujali maslahi, hivyo kanisa linawaomba kuhakikisha watoa rushwa hawapati nafasi hata kama wametumia mamilioni ya fedha," aliongeza.

Aidha, alisema kwa waumini ambao wanaopokea rushwa waonywe kwa kuwa wanatengeneza uongozi wenye rushwa.

Katika hatua nyingine, Askofu Mchopa aliwataka wagombea wa vyama vya siasa ambao waliokosa nafasi kutolipa kisasi kwa waliokuwa wakiwajadili kwenye mchakato wote wa kuwapitisha.

"Mungu mwenyewe ndiye anayewaweka viongozi madarakani kwa mapenzi yake na siyo kwa kuwapitisha kwa njia za rushwa," alisema.

Akizungumza na viongozi waliosimikwa wa kanda hiyo ya kati, Askofu huyo aliwataka kutambua nafasi hizo wamepewa kuwatumikia Watanzania bila kujali itikadi za dini, siasa, kabila au rangi.

"Kuongoza watu si kwa ubabe bali ni kwa unyenyekevu, hivyo kwa nafasi mlizokabidhiwa ni lazima mtambue kuwa mnatakiwa kuwajibika na kusikiliza changamoto mbalimbali za waumini mnaowaongoza bila kujali itikadi za kidini na kisiasa," alisema.

Aliwataka viongozi wa kanisa hilo kuhimiza waumini wao kufanya kazi kwa bidii ili kujiinua kimapato.





# Wanaoishi na VVU waahidiwa pikipiki

**Na Nebart Msokwa,** MBOZI

KATIBU Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Uwekezaji, Doroth Mwaluko, ameahidi kukipatia msaada wa pikipiki kikundi wezeshi cha watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi cha Jitegemee kilichopo katika Kijiji cha Ichesa wilayani Mbozi katika Mkoa wa Songwe ili kukirahisishia utendaji kazi.

Alitoa ahadi hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa anazungumza na wanakikundi hao alipofanya ziara ya kukagua miradi ya kikundi hicho ambayo inatekelezwa na Shirika la Watu VVU (NACOPHA) kupitia Mradi wa Sauti Yetu unaofadhiliwa na Shirika la Misaada la Marekani (USAID).

Alisema pikipiki hiyo itawasaidia wanakikundi hao kwenda kutoa elimu ya UKIMWI kwa wananchi pamoja na kusaidia kusambaza dawa za kufubaza Virusi vya Ukimwi (ARVs).

Alisema kikundi hicho ni miongoni mwa vikundi vinavyofanya vizuri kwenye miradi na kwamba ndiyo sababu iliyomvutia kukizawadia pikipiki ili kukiwezesha kupata mafanikio zaidi.

**Pikipiki hiyo itawasaidia wanakikundi hao kwenda kutoa elimu ya UKIMWI kwa wananchi pamoja na kusaidia kusambaza dawa za kufubaza Virusi vya Ukimwi (ARVs).**

"Mmesema hamna chombo cha usafiri hapa, sasa mimi nitawaletea pikipiki moja ambayo ninaamini itawasaidia kwenye majukumu yenu, nimeridhika na utekelezaji wa miradi hii na muendelee hivihivi mtafika mbali na mtakuwa na maendeleo mazuri kuliko hata wasio na VVU," alisema Mwaluko.

Aidha, Katibu Mkuu huyo alikichangia kikundi hicho Sh. 1,000,000 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa ofisi na ukumbi wa mikutano ambao unaendelea kijijini hapo.

Vilevile, alimtaka Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mahenje kuhakikisha kijiji cha Ichesa kinakuwa na ofisa ugani ambaye atakisaidia kikundi hicho kwenye masuala ya kilimo na mifugo ili wazalishe kitaalamu na kwa tija zaidi.

Akiwasilisha taarifa ya kikundi hicho, Sophia Nyungu, katibu alisema kikundi hicho kilianzishwa mwaka 2013 na kusajiliwa kisheria kikiwa na wanachama 13, lakini kwa sasa kina wanachama 37 ambao wanawake ni 26 na wanaume 11. Alisema kikundi hicho kinafanya shughuli mbalimbali ikiwamo kuhamasisha jamii kupima na kuhakikisha wanaobainika kuwa na maambukizi wanaingizwa kwenye matumizi ya dawa za kufubaza virusi hivyo.

Kadhalika, alisema kikundi hicho kinafanya kazi ya kutoa elimu kwa vijana kuacha matumizi ya dawa za kulevya na ulevi wa kupindukia kwa maelezo kuwa vitendo hivyo pia huchochea maambukizi katika jamii.

Nyungu alisema kikundi hicho kinajishughulisha na shughuli za kilimo na ufugaji na kwamba kina nguruwe 15, mbuzi 10, kuku 10 na ng'ombe mmoja na kwamba kinakusudia kukodi mashamba ekari tatu ambazo mbili ni kwa ajili ya kilimo cha mahindi na moja kwa ajili ya viazi.

Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, John Palingo, alisema kikundi cha Jitegemee Ichesa ni miongoni mwa vikundi vinavyofanya vizuri kwenye konga ya Mbozi.

Alisema atahakikisha kikundi hicho kinaendelea kustawi ili kiendelee kuwa kioo kwa jamii zingine mkoani humo kwa maelezo kuwa kinasaidia hata kuwalea watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu.



Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Uwekezaji, Doroth Mwaluko (wa pili kulia), akikagua baadhi ya bidhaa zinazozalishwa na vikundi vya watu wanaoishi na VVU, zikiwamo unga wa lishe na mikeka mjini Mbozi, mkoani Songwe wikiendi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wanawake Rungwe wataka ujenzi zahanati

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WANAWAKE wakazi wa Kijiji cha Swaya katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, wameiomba serikali iwasaidie kukamilisha ujenzi wa zahanati ya kijiji hicho, ili waondokane na adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya afya.

Wakizungumza na Nipashe jana, walisema wamejenga zahanati hiyo kwa nguvu zao kuanzia msingi mpaka wameezeka lakini wameishiwa nguvu za kumalizia na wanadai kwa kutegemea michango yao watachelewa kukamilisha.

Mmoja wa wananchi hao, Leah Ibanda, alisema wanawake wa kijiji hicho wamekuwa wakilazimika kusafirishwa kwa kutumia pikipiki za abiria maarufu kwa jina la bodaboda kwenda kujifungulia katika Hospitali ya Misheni ya Igogwe. Alisema wengi wamekuwa wakijifungulia njiani kutokana na barabara hiyo kuwa mbovu na wakati mwingine wamekuwa wakiwapoteza watoto wao.

"Tunaomba serikali itusaidie kwa sababu wakati mwingine tukifika hospitali tunajifungua kwa operesheni kwa hiyo inakuwa tatizo kurudi tena nyumbani kwa pikipiki umbali ambao ni zaidi ya kilomita 15," alisema Leah.

Naye Sophia Mwambungu, alisema kitendo cha kijiji hicho kukosa zahanati kinawafanya watumie muda mwingi kusafiri kwenda kutafuta huduma za afya badala ya kufanya shughuli za maendeleo ikiwamo kilimo ambacho ndio tegemeo kwa uchumi wao. Alisema katika kijiji hicho wanalima zaidi viazi mviringo ambavyo vinahitaji uangalizi wa karibu na kwamba familia inapokuwa na mgonjwa katika Hospitali ya Igogwe muda mwingi unatumika huko badala ya kusimamia mazao.

Alisema endapo zahanati yao itakamilika, itakuwa rahisi kuwahudumia wagonjwa na kufanya shughuli za uzalishaji, hivyo kuachana na safari ndefu ya kwenda Igogwe.

# Sababu kasi ya UKIMWI kwa wasichana yatajwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IMEELEZWA kuwa asilimia 80 ya vijana wanaopata maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU) nchini ni wasichana wenye umri kati ya miaka 15 na 24 hali ambayo inadaiwa kuwa inasababishwa na baadhi ya yao kuishi katika mazingira magumu.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Kudhibiti UKIMWI nchini (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Mbeya wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya namna ya kujikinga na maambukizi ya VVU kwa vijana wa kike, ambapo alisema wengi wa vijana hao wanakuwa hawana fursa za kujiingizia kipato.

Alisema takwimu hizo zinaonyesha asilimia 40 ya watu wote wanaopata maambukizi mapya ya virusi hivyo ni vijana na kwamba vijana wa kike ndio waathirika wakubwa zaidi kuliko wa kiume ambao ni asilimia 20 pekee.

"Kwa siku yanatokea maambukizi mapya ya VVU 200 ambayo asilimia 40 yake ni vijana na kati ya vijana hao wa kike ni asilimia 80, kwa hiyo kwa siku wasichana 64 wanasadika kupata maambukizi hali ambayo ni kazi kubwa," alisema Dk. Maboko.

Aliiomba jamii kushirikiana na serikali kwenye vita dhidi ya VVU ili kuhakikisha malengo ya kufikia 95 tatu yanafikiwa ambayo ni kufikia asilimia 95 ya utambuzi wa watu wanaoishi na VVU, kufikia asilimia 95 ya kuwaingiza watu wanaoishi na VVU kwenye matumizi ya dawa za kufubaza virusi na asilimia 95 ya wanaotumia dawa hizo wawe wamefubaza.

Mtendaji Mkuu wa Shirika la Walter Reed Tanzania ambalo ndilo linafadhili mafunzo hayo, David Maganga, alisema mbali na vijana hao kupewa elimu ya kujikinga na maambukizi, pia wanatakiwa kusaidiwa kiuchumi.

Alisema wengi huwa wanajiingiza kwenye vitendo ambavyo vinawasababishia maambukizi kwa sababu wanakuwa hawana shughuli za kujiingizia kipato na hivyo kujikuta wanatafuta riziki kwa kushiriki ngono.

Alisema vijana hao wakianzishiwa miradi ya kujiingizia kipato, watakuwa salama zaidi kuliko wakaishia kupatiwa elimu ya kujikinga na VVU pekee.

"Tunatoa elimu ya kujitambua, msichana huyu anaweza akawa anajitambua lakini kama hatajengewa uwezo wa kujitegemea mwenyewe kiuchumi anaweza akarudi tena kwenye mazingira aliyokuwapo awali," alisema Maganga.

Aliwaomba wadau kushirikiana na serikali katika kuhakikisha vijana hao wanawezeshwa kiuchumi ili wawe katika mazingira salama.

Aidha, aliwataka wasichana wanaopata elimu hiyo ya kujikinga na maambukizi kuwasaidia wenzao mitaani kwa kuwafundisha mbinu ambazo wanazipata kwenye mafunzo hayo ili na wao wanufaike.



# Chanjo watoto yafanikiwa licha tishio corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

LICHA ya Tanzania kukumbwa na ugonjwa wa corona, wazazi wengi wamepeleka watoto wao kupata chanjo za kujikinga na maradhi mbalimbali ikiwamo surua.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, mratibu wa chanjo Zanzibar, Yussuf Haji Makame, alisema chanjo iliendelea vizuri katika vituo vya afya wakati wa janga la corona.

Mratibu huyo alisema pamoja na kuwapo kwa ugonjwa wa corona, wazazi na walezi waliitikia wito wa kuwapeleka watoto wao kupata chanjo mbalimbali zinazowahusu.

"Hapa katikati tulilega kidogo hasa mwezi wa Machi mwishoni mlipuko wa corona ulipotokea Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, lakini zoezi hilo liliendelea vyema hadi sasa," alisema.

Alisema kwa kawaida mtoto anapozaliwa kuanzia siku moja hadi mwaka mmoja na nusu analazimika kupata chanjo za aina tofauti za kinga dhidi ya maradhi mbalimbali ikiwamo surua.

Alisema mtoto hadi kufikia umri wa miaka mitano anatakiwa kupimwa ili kujua maendeleo ya ukuaji wake. Akizungumzia janga la corona na chanjo za watoto, alisema kuwa kundi la watoto limenusurika kwa kiasi kikubwa na maambukizi ya corona.

Kadhalika, alisema si Zanzibar pekee, karibu nchi nyingi zilizopata maambukizi hayo hayakuwagusa watoto.

"Ni kesi chache sana za watoto waliokumbwa na maambukizi ya corona na hii nadhani hizi chanjo za watoto zimewasaidia kwa kiasi kikubwa sana kuwanusuru na maambukizi ya corona," alisema.

Alisema hata kama mama ataugua corona, lakini watoto walinusurika, hizi chanjo zinasaidia sana ingawa hakuna utafiti uliofanyika," alisema.

Hata hivyo, aliwataka wazazi kutodharau umuhimu wa chanjo na kuwataka kuwapeleka watoto wao kwenye chanjo za kawaida na za kampeni maalumu.

Alizitaja chanjo hizo kuwa ni pamoja na BCG ya kinga dhidi ya kifua kikuu, polio ambayo inajumuisha magonjwa ya kifaduro, donda koo, homa ya ini, homa ya uti wa mgongo na kinga dhidi ya homa ya nimonia na surua.

Yussuf alisema ipo haja kwa wazazi na walezi kujua umuhimu wa chanjo kwa watoto wao ambazo zinatolewa bure na serikali hata kama vituo vya afya vya binafsi hupata kutoka serikalini.

Alisema kwa kiasi kikubwa maradhi mbalimbali yanayowasibu watoto yamepungua jambo ambalo linaonyesha jamiii kuunga mkono serikali.

"Lengo ni kuwapata watoto wenye afya njema na ndio maana serikali ikaona umuhimu wa kuwapa chanjo watoto bila malipo ili kuwanusuru na magonjwa mbalimbali," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Zanzibar Youth Forum, Maulid Suleiman, alisema ili taifa liweze kuwa na vijana imara ni lazima watoto wapate chanjo za kujikinga na maradhi kwasababu ndio vijana wa baadaye wa kujenga taifa.

# Dk. Shein: Zanzibar ina sifa zote za jiji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ameutaka uongozi wa Mkoa wa Mjini Magharibi na manispaa zake kuhakikisha mji wa Zanzibar unakuwa safi kwa sababu sasa ni jiji.

Dk. Shein alisema jana, Ikulu alipokutana na uongozi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), wakati ilipowasilisha taarifa ya utekelezaji wa Mpango kazi wa mwaka 2019/2020 na 2020/2021.

Alisema kuna haja ya kuweka mikakati maalum ili mji wa Zanzibar uendelee kuvutia na kufikia malengo ya kuufanya kuwa jiji kutokana na sifa ulizonazo. Pia, alisema ipo haja kwa uongozi wa mkoa kuangalia suala la usafi hasa katika masoko na barabarani ambayo yamevamiwa na wafanyabiashara na kusababisha uchafuzi wa mazingira na kuepusha ajali za barabarani.

**Licha ya serikali kubuni mpango wa masoko mapya, katika eneo la soko la Mwanakwerekwe kumeendelea kuwa na msongamano mkubwa wa wafanyabiashara ambao hufanya shughuli zao pembezoni mwa barabara.**

Aliutaka uongozi wa mkoa huo kufanya kazi kiserikali kwa kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo ili biashara zote zifanywe kwa kufuata taratibu na sheria.

Alisema licha ya serikali kubuni mpango wa masoko mapya, katika eneo la soko la Mwanakwerekwe kumeendelea kuwa na msongamano mkubwa wa wafanyabiashara ambao hufanya shughuli zao pembezoni mwa barabara.

Alisema ipo haja ya kuandaa utaratibu maalum wa kuwaweka wafanyabiashara katika mazingira mazuri pale wanapowaondoa kutoka eneo moja kwenda eneo jingine kwa ajili ya kufanya biashara zao.

Alipongeza hatua za kuanzisha mnada mkuu katika soko jipya la Jumbi hali inayosaidia kuondoa msongamano wa wafanyabiashara sokoni.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Haji Omar Kheri, alisema ofisi imeendelea kuhudumia shule 327 za maandalizi na msingi kwa kutoa huduma ya ufundishaji na kujenga mazingira mazuri ya kujifundishia.

Alisema kuwa ununuzi wa madaftari 4,624,846 ya wanafunzi 325,009, madaftari 5,500 ya mahudhurio na kadi 50,000 za maendeleo ya wanafunzi umefanyika na kusambazwa kila wilaya za Unguja na Pemba na kuwawezesha wanafunzi wote kuwa na madaftari ya kuandikia bila ya gharama za wazazi.

Alisema huduma za tiba na kinga ya afya ya msingi pamoja na huduma za afya ya mama na mtoto zimetolewa katika vituo 154 vya afya Unguja na Pemba chini ya usimamizi imara wa Serikali za Mitaa.



Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi (wa tatu kulia), na uongozi wa taasisi za ujenzi mazingira na serikali ya mkoa Mjini Magharibi, wakikagua mmomonyoko wa ardhi katika eneo la pembezoni mwa ufukwe wa bahari wa Mazizini, jana. **PICHA: OMPR – ZNZ**

# Watakiwa kuzingatia miiko kuripoti magonjwa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WANACHAMA wa klabu ya waandishi wa habari Zanzibar (ZPC), wametakiwa kuandika habari za ugonjwa wa milipuko kwa kuzingatia miiko na maadili ya uandishi ili kuepuka kuwatia taharuki wananchi.

Akifungua mafunzo kwa wanachama wa klabu hiyo kuhusu magonjwa ya milipuko, pamoja na mkutano mkuu wa klabu hiyo, Mkurugenzi wa Manispaa Magharibi 'A' Unguja, Amour Ali Mussa, alisema hatua hiyo itasaidia kuwafanya wananchi kuondokana na hofu kubwa na kushindwa kuendelea na harakati zao.

Alisema kuwa ugonjwa wa corona ulipoingia nchini wananchi walikuwa na hofu kubwa, lakini kalamu na sauti za waandishi wa habari zilichangia kuondoa taharuki kwa wananchi baada ya viongozi wa nchi kuwatoa hofu.

Aliwataka waandishi wa habari kuilinda tasnia ya habari dhidi ya wasiokuwa na maadili na kuwafichua ili kwenda sambamba na misingi ya tasnia hiyo kwa manufaa ya taifa.

Akiwasilisha mada kuhusu ugonjwa wa Covid-19, Mkuu wa Kitengo cha Elimu ya Afya, Halima Ali Khamis, aliwataka waandishi kuendelea kuhamasisha jamii kuchukua tahadhari kwa kuwa ugonjwa huo bado upo nchini licha ya kupungua kwa kiasi kikubwa.

Aliwataka wananchi kuendelea kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya ikiwamo kuvaa barakoa katika mikusanyiko ya watu wengi.

Waandishi wa habari wa klabu hiyo walifanya uchaguzi na kumchagua Abdallah Abrahman Mfaume, kuwa Mwenyekiti wa ZPC, Tabia Makame, Makamu Mwenyekiti, Mwinyimvua Abdi Nzukwi, Katibu Mkuu na Mwajuma Juma, Naibu Katibu Mkuu.

Pia walimchagua Rahma Suleiman kuwa mwekahazina wa klabu hiyo na wajumbe wa kamati tendaji ni Amina Mchezo, Aziza Hassan, Zuhura Msabah, Maulid Kipevu, Saleh Hassan na Mwarabu Mmadi.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa uchaguzi huo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Dk. Yussuf Mnemo, aliwataka wanachama wa klabu hiyo waliokosa nafasi kutokuwa na kinyongo na badala yake kushirikiana na viongozi waliochaguliwa ili kuiletea maendeleo klabu hiyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.
Mawasiliano yetu Dar es salaam – 0768 928 516. Arusha – 0677 226 960.

## NYUMBA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA, Nyumba ya Gorofa 1, inauzwa na fremu za biashara, umeme na maji. Inafaa kwa kuishi na kwa biashara. Mawasiliano: 0757 079057.**

## NIP ASHE NI JIB U LAK O

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 231/2020**

**Ombi la MWARABU AHMED MUMBA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu FARIDA HABIBU MUMBA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 28/08/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 14/08/2020.

Tarehe 14/8/2020
Sahihi ya Hakimu

115861302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakam ya mwanzo MJINI TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi 126 20 20**

**Ombi la SAIDI MACHUNDA ADAM kuteuliwa Msimamizi wa mirathi ya marehemu ADAM DAUDI BUNYANZA**

**Kwa yeyote anayehusika**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 17/9/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 17/8/20 20

115861502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi 95 /2020.**

**Ombi la JOVITA SIMON KIIZA kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi Marehemu BONIFACE JULIUS TIBAIJUKA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 21/8/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 17/8/2020.

Sahihi ya Hakimu

115861002

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF MOSHI AT MOSHI**

**EXTENDED JURDISTICTION LAND APPEAL NO. 24 OF 2020**

**EDWARD HELGARD SAM APPLELLANT**
**VERSUS**
**RRAY AUCTIONEERS & COURT BROKERA**
**RESPONDENT**
**TO : GRAY AUCTIONEERS & COURT BROKERS**
**NOTICE OF DATE MENTION/HEARING**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for MENTITION/HEARING on 20th the day of Aug 2020 at 9:00am Before Honourable B.T. Maziku SRM .
**YOU ARE** required to appear in this Court without fail and you must produce to that day all documents upon which you intend to reply on support of your case.

**GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT , this 10 day of August 2020**

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

115861102

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF MOSHI AT MOSHI**

**EXTENDED JURDISTICTION LAND APPEAL NO. 24 OF 2020**
**EDWARD HELGARD SAM APPLELLANT**
**VERSUS**
**PRIDE TANZANIA MOSHI BRANCHI RESPONDENT**
**TO PRIDE TANZANIA –MOSHI BRANCHI**
**NOTICE OF DATE MENTION/HEARING**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for MENTITION/HEARING on 20th the day of Aug 2020 at 9:00am Before Honourable B.T. Maziku SRM .
**YOU ARE** required to appear in this Court without fail and you must produce to that day all documents upon which you intend to reply on support of your case.

**GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT, this 10day of August 2020**

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

115861102

---

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

---

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katik a gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Wapanga kufanya maandamano kupinga uchaguzi

**MINSK,** Belarus

MAANDAMANO mapya yanatarajiwa kufanyika tena nchini Belarus baada ya maelfu ya watu kuandamana wakimtaka Rais Alexander Lukashenko, aondoke madarakani.

Viongozi wa upinzani walitoa wito wa maandamano, huku hasira zikiendelea kuongezeka juu ya taarifa za polisi kutumia nguvu kupita kiasi pamoja na madai ya udanganyifu katika uchaguzi wa Agosti 9.

Lakini, Rais Lukashenko ambaye anadai alipata ushindi wa kishindo bado anakaidi wito wa kijiuzulu.

Jumapili, Rais Lukashenko alitoa wito kwa wafuasi wake kutetea nchi yao na uhuru wao.

Hata hivyo, waandamanaji nchini humo walijitokeza kwa wingi huku wenyeji, kulingana na tovuti ya habari inayojitegemea ya -Tut.by, ikisema kwamba maandamano hayo ndio makubwa zaidi kuwahi kufanyika katika historia ya Belarus.

Ghadhabu imekuwa ikiongezeka tangu Tume ya Uchaguzi iliposema kuwa Rais Lukashenko, ambaye amekuwa madarakani tangu 1994, ameshinda uchaguzi kwa asilimia 80.1 ya kura zote zilizopigwa, huku kiongozi wa chama kikuu cha upindani, Svetlana Tikhanovskaya, akipata asilimia 10.12 ya kura zilizopigwa.

Tikhanovskaya, ambaye alikimbilia Lithuania baada ya kukataa matokeo hadharani, alisema kuwa maeneo ambapo kura zilihesabiwa vizuri alishinda kwa kati ya asilimia 60 na 70. Katika ujumbe kwa njia ya video Jumatatu, Tikhanovskaya alisema kwamba yuko tayari kuwa kiongozi wa Taifa ili kurejesha amani na hali ya kawaida, kuachilia wafungwa wa kisiasa na kujitayarisha kwa uchaguzi mpya.

Wakati huohuo, baadhi ya watu 6,700 wamekamatwa tangu kuanza kwa maandamano, na wengi wamezungumzia mateso waliopitia mikononi mwa maofisa wa usalama.

Wafanyakazi wa umma washiriki mgomo jana, huku chombo cha habari kikionyesha chumba cha kusomea habari bila wafanyakazi.

Wiki iliyopita, wafanyakazi katika kampuni zinazoendeshwa na serikali, waliungana na waandamanaji wengine huku maandamano zaidi yakipangwa kufanyika wiki hii, kama njia moja wapo ya kuongeza shinikizo kwa Rais Lukashenko.

Mikutano ya upinzani ilifanyika katika mji mkuu wa nchi hiyo wa Minsk, huku vyombo vya habari vikisema kwamba karibu watu 31,000 walishiriki kwenye mkutano wa kuunga mkono serikali.

Alizungumza na wafuasi wake, Rais Lukashenko alisema Belarus itakufa kama Taifa likiwa uchaguzi utarudiwa tena. **BBC**

# Mawaziri wa Kenya wapewa likizo siku 10

**NAIROBI,** Kenya

BARAZA la Mawaziri nchi Kenya limeanza rasmi mapumziko ya siku 10, kama alivyoagiza Rais Uhuru Kenyatta.

Hatua hiyo imezua hisia tofauti miongoni mwa wananchi, huku baadhi yao wakieleza kuwa mabadiliko yananukia kwenye Baraza la Mawaziri.

Agizo hilo la Rais Kenyatta limezua hisia mbalimbali kuwa huenda Rais Kenyata akatumia fursa hiyo kufanya mabadiliko kwenye baraza hilo.

Watu wa karibu na Rais Kenyatta wamenukuliwa wakieleza kuwa muda wa kufanya mageuzi hayo umewadia.

Kwa upande wa pili, baadhi ya wandani wa kisiasa wa kiongozi wa upinzani Raila Odinga wamekuwa wakielezea wasiwasi wao kuhusu maridhiano kati ya Rais Kenyata na kiongozi wao.

**Taarifa zimeeleza kuwa Rais Kenyatta huenda akawasogeza karibu wandani wake wa kisiasa ili kulipa nguvu.**

Viongozi hao wawili walifikia mwafaka kushirikiana Machi mwaka 2018, kwa kile kinachojulikana kama salamu za kheri, zilizosaidia kupunguza joto la kisiasa na mpasuko uliokuwapo kati ya Wakenya.

Hata hivyo, Mkuu wa Idara ya Huduma za Umma, Joseph Kinyua, alipuuza tetesi za kufanyika kwa mabadiliko kwenye Baraza la Mawaziri. Badala yake alisisitiza kuwa kiongozi wa Taifa hilo ana imani na kikosi chake.

Taarifa mbalimbali zimeeleza kuwa Rais Kenyatta huenda akawasogeza karibu wandani wake wa kisiasa ili kulipa nguvu mpya baraza hilo.

Inasadikika kuwa upande wa upinzani unatiwa shaka na hali ya kisiasa ukizingatia kuwa uchaguzi mkuu umepangwa kufanyika mwaka 2022.

Vyama vya kisiasa tayari vimeanza maandalizi ya uchaguzi mkuu ujao.

Mkuu wa Idara ya Huduma za Umma, Joseph Kinyua, aliweka bayana kuwa mawaziri hawatakuwa na majukumu yoyote wakati huu wa mapumziko. Mapumziko hayo yatafikia kikomo Agosti 28, mwaka huu. **DW**




Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, akiwa katika moja ya tukio la kuwahutubia wananchi, huku akilipa likizo Baraza la Mawaziri kwa muda wa siku 10. **PICHA: REUTERS**

# Burundi kuzidai fidia Ujerumani, Ubelgiji

**BUJUMBURA,** Burundi

NCHI ya Burundi imezitaka Ujerumani na Ubelgiji kulipa fidia ya Euro bilioni 36 kutokana na ukoloni.

Baraza la seneti la nchi hiyo limeunda jopo la wataalamu watakaochunguza madhara yaliyotokana na ukoloni na kushauri kuhusiana na kiasi cha fidia.

Kituo cha redio cha Ufaransa RFI kinasema mara tu kiasi cha fidia kitakapoamuliwa, Burundi inapanga kupeleka mapendekezo hayo kwa serikali za Ujerumani na Ubelgiji.

Nchi hiyo pia inapanga kuitisha turathi zake za kihistoria zilizoibwa, kutoka kwa nchi za Ulaya.

Burundi ilikuwa koloni la Ujerumani kutoka mwaka 1890 na baada ya vita vya kwanza vya dunia nchi hiyo ikawa koloni la Ubelgiji mpaka ilipopata uhuru mwaka 1962.

Katika enzi za ukoloni, nchi hizo zilichochea mgawanyiko kati ya Wahutu na Watutsi.

Jambo hili lilichangia kuzuka kwa mapigano mabaya baina ya makabila hayo mawili katika miaka ya 1970 na mapigano mengine ya wenyewe kwa wenyewe yaliyodumu kwa miaka 12 kuanzia mwaka 1993. Karibu watu 300,000 walifariki dunia katika mapigano hayo.

Serikali ya Ubelgiji ilikuwa na mpango wa kuwateka nyara watoto kutoka Burundi na Congo katika miaka ya 1940 na 1950. Mwaka 2009, Ubelgiji iliomba msamaha rasmi kwa vitendo hivyo.

Ingawa haijulikani sana katika masuala ya ukoloni, Ujerumani wakati mmoja ilikuwa ndiyo taifa la nne duniani lenye nguvu kubwa zaidi ya ukoloni.

Pamoja na eneo lililoitwa German East Africa lililojumuisha Rwanda na sehemu za Tanzania pamoja na Burundi, Ujerumani ilikuwa na maeneo mengine pia kama nchi ambazo sasa ni Ghana na Namibia.

Serikali ya Ujerumani imekuwa katika meza ya mazungumzo na Namibia tangu 2015 kwa kuwa nchi hiyo inataka fidia ya fedha pamoja na kuombwa msamaha rasmi na Ujerumani kwa hasara iliyopata na uhalifu uliofanywa katika kipindi cha ukoloni.

Ubelgiji inapanga kuunda jopo la wataalamu kuishauri serikali kuhusiana na namna ya kukabiliana na historia yake ya kikoloni. **DW**

# LACAZETTE AWANIWA JUVENTUS




**TURIN,** Italia

JUVENTUS inawania kumsajili straika wa Arsenal, Alexandre Lacazette, kwa mujibu wa Sky in Italia.

Straika wa Wolves, Raul Jimenez pia yupo kwenye orodha ya wanaowaniwa na miamba hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, huku nyota wa Atalanta, Duvan Zapata, mkali wa Atletico Madrid, Alvaro Morata, mchezaji wa Napoli, Arkadiusz Milik na mshambuliaji wa Roma, Edin Dzeko pia wakiwaniwa.

Mshambuliaji wa sasa wa Juve, Gonzalo Higuain anatarajiwa kuondoka, akiwa amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake.

Andrea Pirlo, ambaye hivi karibuni alichukua mikoba ya ukocha baada ya kufukuzwa kwa Maurizio Sarri, anatafuta mshambuliaji mpya wa kati wa kuwa patina wa Cristiano Ronaldo na Paulo Dybala.

Arsenal tayari imekamilisha usajili wa Willian kwa mkataba wa miaka mitatu baada ya kuondoka Chelsea.



# *Silva awajia juu mashabiki Liverpool*

**MANCHESTER,** England

BERNARDO Silva amewajia juu mashabiki wa Liverpool na kuwaita "dhaifu" huku akiwashauri watumie muda wao vizuri badala ya kujihusisha na mambo yasiyowahusu.

Silva alikuwa benchi na hakutumika wakati Manchester City walipomaliza msimu wa 2019-20 kwa machungu kwa kuchezea kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Lyon kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumamosi.

Wakiwa wamemaliza ligi kwa kupitwa pointi 18 na mabingwa Liverpool, kuondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, lilikuwa pigo kubwa zaidi kwa City.

Silva awali alionyesha kusikitishwa kwake na msimu mbaya wa 2019-20 na akaomba radhi kwa mashabiki wa City kupitia kwenye mtandao wa kijamii wa Instagram.

Lakini haraka mashabiki wa Liverpool wakaaanza kumkebehi nyota huyo wa kimataifa wa Ureno.

"Kwa mashabiki wote wa Liverpool hamna cha kufanya zaidi ya kuja kwenye akaunti ya mchezaji wa Man City, nawasikitikia," aliandika.

"Dhaifu nyie... nendeni mkasherehekee ubingwa na kujaribu kunywa bia na marafiki zenu au kusoma vitabu. Acheni kuingia kwenye akaunti yangu na kuandika mambo ya ajabu. Hii ni aibu kwenu."

# Maguire: Hatukustahili kufungwa na Sevilla

**COLOGNE,** Ujerumani

HARRY Maguire amedai "timu bora imepoteza" wakati Manchester United ikitupwa nje kwenye mashindano ya Kombe la Ligi ya Europa na Sevilla katika hatua ya nusu fainali.

Luuk de Jong, ambaye alicheza pale Newcastle United miaka sita iliyopita, alionyesha namna gani anaweza kutafuta ushindi baada ya kuwawezesha miamba hao wa Hispania kupata ushindi wa 2-1 mjini Cologne.

Penalti ya mapema ya Bruno Fernandes ilisawazishwa na Suso, na De Jong akafunga bao la ushindi dakika ya 78.

"Ni ngumu. Vijana wameumia," alisema nahodha Maguire akinukuliwa na BT Sport mara baada ya mchezo huo.

"Tulitengeneza nafasi za kutosha na tulitakiwa kushinda mchezo huu. Timu bora imepoteza na wametuadhibu kwa kushindwa kutumia nafasi zetu vizuri.

Maguire pia alisema Man United lazima ijiimarishe zaidi kwa sababu walishindwa kutumia nafasi zao vizuri na hivyo kujikuta wakipoteza nafasi nzuri zaidi kwao.



HABARI MICHEZO

# DE BRUYNE MCHEZAJI BORA WA MSIMU EPL




**LONDON,** England

NYOTA wa Manchester City, Kevin De Bruyne, ametwaa tuzo ya mchezaji bora wa msimu 2019-20.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alipewa tuzo hiyo baada ya kupigiwa kura na mashabiki, manahodha wa klabu za England na wachambuzi wa soka.

De Bruyne aliwashinda nyota watatu wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold, Jordan Henderson na Sadio Mane - pamoja na Danny Ings, Nick Pope na Jamie Vardy.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, alikuwa nguzo ya Man City wakati ikimaliza nafasi ya pili kwenye msimamo nyuma ya Liverpool, akifunga mabao 13 na kutoa pasi za mwisho 20, ambapo aliifikia rekodi ya Thierry Henry ya kutoa asisti nyingi kwa msimu mmoja ambayo aliiweka msimu wa 2002-03.

Katika tuzo hiyo, nyota wa Liverpool, Alexander-Arnold alishinda kama mchezaji bora kijana wa msimu na Jurgen Klopp alishinda kama kocha bora.

Kiungo huyo ni mchezaji wa tatu wa Ubelgiji kushinda tuzo hiyo baada ya mchezaji mwenzake wa zamani, Vincent Kompany kushinda msimu wa 2011-12 na nyota wa zamani wa Chelsea, Eden Hazard kushinda msimu wa 2014-15.

# Koeman kumrithi Setien Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

RONALD Koeman (pichani) ndio anaongoza kupewa nafasi ya kuwa kocha mpya wa Barcelona wakati Quique Setien akitarajiwa kufukuzwa.

Setien anatarajiwa kufukuzwa baada ya kikao cha Mkurugenzi wa Ufundi, Eric Abidal ndani ya siku chake zijazo kutokana na kuchezea kichapo cha mabao 8-2 kutoka kwa Bayern Munich kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Koeman – mchezaji wa zamani wa Barcelona, anatajwa kuwa chaguo sahihi kwa Rais wa klabu hiyo, Josep Maria Bartomeu.

Barca italazimika kulipa fidia ili kumpata Koeman ambaye kwa sasa ni kocha mkuu wa timu ya Taifa ya Uholanzi.

Kocha wa zamani wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino pia anatajwa kuwa kwenye nafasi nzuri ya kupewa kazi hiyo.

Yeye anatajwa kama chaguo la Mkurugenzi, Ramon Planes, ambaye alifanya naye kazi wakati akiwa kule Espanyol.







# Solskjaer ataka usajili mpya

**COLOGNE,** Ujerumani

MANCHESTER United inatakiwa kufanya usajili wa maana baada ya kupoteza kwenye nusu fainali ya Kombe la Ligi ya Europa kwa kufungwa na Sevilla mabao 2-1, kwa mujibu wa Kocha Mkuu, Ole Gunnar Solskjaer.

Solskjaer anataka kukiimarisha zaidi kikosi chake akiwa tayari amepata matunda ya kumsajili Bruno Fernandes.

Fernandes, ambaye alisajiliwa Januari kutoka Sporting CP - alifunga penalti ya mapema dhidi ya Sevilla, lakini Suso na Luuk de Jong wakaipa ushindi wa 2-1 timu hiyo ya Hispania mjini Cologne.

United imekuwa ikihusishwa kwa muda mrefu na nyota wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho, lakini Solskjaer alikataa kuzungumzia hilo.

"Tumeingia kwenye kipindi cha majira ya joto na tunapaswa kufanya usajili," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Tuna wiki nyingi za kujiimarisha kabla ya kuingia tena kwenye msimu mpya. Ni changamoto kwetu, lakini tunatakiwa kufanya usajili wa maana.

"Tutatakiwa kujipanga vizuri na kutafuta wachezaji ambao watatusaidia kuijenga timu yetu."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# AUBAMEYANG AKUBALI KUSAINI MKATABA MPYA

## Dili hilo litatangazwa siku chache zijazo, hivyo kuvunja uvumi kuwa anataka...

**LONDON,** England

PIERRE-Emerick Aubameyang anakaribia kumaliza uvumi kuhusu majaliwa yake kwa kusaini mkataba mpya na Arsenal.

**Sky Sports News iliripoti wiki iliyopita namna gani straika huyo wa kimataifa wa Gabon anakaribia kufikia makubaliano, wakati mkataba wake wa sasa ukiwa unamalizika msimu ujao.**

Aidha, Sky Sports Italia imeripoti kwamba, kusaini mkataba mpya kwa Aubameyang kutatangazwa siku chache zijazo. Majaliwa ya Aubameyang yalipamba vyombo vya habari baada ya kuingia kwenye mwaka wake wa mwisho wa mkataba wake.

Alifunga mabao 22, kwenye Ligi Kuu ya England na akafunga mara mbili kwenye fainali ya ushindi ya Kombe la FA dhidi ya Chelsea.

Tangu alipojiunga na Arsenal akitokea Dortmund Januari mwaka 2018, amefunga mabao 54 kwenye mechi za Ligi Kuu 85.

Kwa sasa ana umri wa miaka 31, na Arsenal imemsajili Willian mwenye umri wa miaka 32 kwa mkataba wa miaka mitatu.

Aubameyang baada ya mchezo wa fainali ya Kombe la FA alikataa kuzungumzia kuhusu majaliwa yake akibainisha kwamba wakati huo ulikuwa ni wa kusherehekea ushindi.

Kocha wake, Mikel Arteta mara kadhaa amenukuliwa akisema kwamba ana matumaini nyota huyo atasaini mkataba mpya na klabu hiyo na hivyo hana shaka kwamba anaweza kuondoka.

## ZISIKUPITE

### MESSI KUONDOKA BARCA

LIONEL Messi ameiambia Barcelona anataka kuondoka klabuni hapo mara moja, huku Manchester City ikiongoza katika kinyang'anyiro cha kumuwania mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 33 raia wa Argentina. ***(Esporte Interativo, via Mirror)***

### THIAGO KIMEELEWEKE LIVER

NYOTA wa Bayern Munich, Thiago Alcantara, amekubalia mkataba wa miaka minne na Liverpool, huku klabu hiyo ya Bundesliga ikitaka ziada ya pauni milioni 30 kwa kiungo huyo wa kati mwenye umri wa miaka 29, raia wa Hispania. ***(RMC Sport, via Mirror)***

### JUVE KWA LACAZETTE, JIMENEZ

MABINGWA wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Juventus wanawafuatilia kwa karibu kutaka kuwasajili mshambuliaji wa Arsenal raia wa Ufaransa, Alexandre Lacazette au mshambuliaji wa Wolves raia wa Mexico, Raul Jimenez, ambao kila mmoja ana umri wa miaka 29. ***(Sky Sports)***

### GRIEZMAN SOKONI BARCA

KLABU ya Barcelona itasikiliza ofa za mshambuliaji wa Ufaransa, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 29, ikiwa ni mwaka mmoja tu baada ya kuwasili hapo akitokea Atletico Madrid kwa pauni milioni 107. ***(Sport via Express)***

### LEICESTER YAMWANIA TIMOTHY

KLABU ya Leicester City inakabiliana na ushindani kutoka kwa Paris St-Germain katika kumuwania mlinzi wa Atalanta na Ubelgiji, Timothy Castagne mwenye umri wa miaka 24. ***(Calciomercato via Leicestershire Mercury)***

### INTER YAMTAKA SMALLING

INTER Milan inamnyatia mlinzi wa Manchester United, Chris Smalling mwenye umri wa miaka 30, na huenda ikalipa kitita cha pauni milioni 20 kwa ajili ya mchezaji huyo aliyekuwa beki wa kati wa England. ***(Metro)***

### JUVE KUMUUZA DYBALA

JUVENTUS iko tayari kumuuza Paulo Dybala,26, huku Manchester United na Tottenham zikionyesha nia ya kutaka kumsajili. ***(Gazetta Dello Sport)***

### LEEDS YAJITOSA KWA ROBIN

MACHO ya Leeds United sasa yapo kwa mlinzi wa Ujerumani na Freiburg, Robin Koch, 24, huku matumaini ya kufikia makubaliano na ambaye alikuwa mlengwa wao mkuu, beki wa kati wa Brighton, Ben White, mwenye miaka 22, yakionekana kudidimia. ***(Telegraph)***

### TRAORE KUTUA CAEN

KIUNGO wa kati wa Manchester United na timu ya Taifa ya Ufaransa, Aliou Traore, 19, yuko tayari kujiunga na Caen kwa mkopo. ***(Goal)***

### HOWE APOTEZEA UKOCHA

KOCHA wa Bournemouth, Eddie Howe, mwenye umri wa miaka 42, hapangi kurudi katika soka hadi Krismasi ambapo atakuwa amepumzika baada ya kuondoka klabuni hapo. ***(Mail on Sunday)***

### NEWCASTLE YAMTAKA ROB

KLABU ya Newcastle United inawania kumsajili mlinzi na nahodha wa Oxford United, Rob Dickie, mwenye umri wa miaka 24. ***(Sun)***

HABARI MICHEZO



Meneja wa NBC Tawi la Chang'ombe, Aliko Mwamusako, akisalimiana na timu ya Wanafunzi wa mwaka wa tatu ya Chuo cha DUCE katika Bonanza la Siku ya Daruso-DUCE lililokuwa mahususi kwa ajili ya kuwaaga viongozi wa Serikali ya Wanafunzi ambao wanamaliza muda wao na kukaribisha uongozi mpya chuoni hapo. Benki ya NBC ndio iliyodhamini bonanza hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NBC YAGEUKIA MICHEZO VYUONI

**Na Mwandishi Wetu**

ILI kuhakikisha michezo nchini inazidi kukua, Benki ya NBC imegeukia sekta hiyo kwa upande wa vyuo, kwa kudhamini Tamasha la Michezo la "Daruso-DUCE Day" katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam.

**Tamasha hilo ambalo hufanyika kila mwaka, lilihusisha mchezo wa mpira wa miguu, mpira wa kikapu, netiboli, mpira wa wavu, riadha na kuvuta kamba.**

Katika tamasha hilo, ambalo lilifanyika Jumamosi iliyopita, lilikuwa mahususi kwa ajili ya kuwaaga viongozi wa Serikali ya Wanafunzi ambao wamemaliza muda wao na kukaribisha uongozi mpya chuoni hapo, hivyo Benki ya NBC ikatumia fursa ya michezo kukutanisha watu kutoka makundi mbalimbali ya kijamii.

Kivutio kikubwa kilikuwa ni mechi ya mpira wa miguu kati wanafunzi wa mwaka wa tatu dhidi ya timu ya mchanganyiko kwa wanafunzi wa mwaka wa pili na wa kwanza, ambayo ilimalizika kwa sare ya bao 1-1 ndani ya dakika 90 kabla ya changamoto ya mikwaju ya penalti kuchukua nafasi yake. Kipa wa timu ya mwaka wa tatu, aliibuka shujaa baada ya kuibebesha timu yake ushindi kutokana na kucheza mikwaju miwili wakati wakishinda kwa penalti 4-2.

Aidha, katika kusaidia maendeleo ya vijana, Benki ya NBC inawalipia gharama za masomo zaidi ya wanafunzi 30 ambao wana changamoto za kifedha chuoni hapo. Programu hiyo inawagharamia wanafunzi kutoka vyuo vitatu zaidi, Chuo cha Udhibiti wa Fedha (IFM), Chuo cha Biashara Dar es Salaam (CBE) na Chuo cha Wanyamapori, MWEKA.

"Sisi kama NBC tawi la Chang'ombe, tumedhamiria kuendeleza uhusiano mzuri tulionao na Chuo cha DUCE ili kuhakikisha tunawasaidia wanafunzi kadri tuwezavyo; na bonanza hili ni miongoni mwa jitihada zetu katika kuimarisha umoja, afya njema na elimu ya fedha. Lengo ni kuwaandaa vijana wanaohitimu wawe na uelewa wa kifedha.

"Ndio maana tumeanzisha "Malengo Account", akaunti maalumu inayomuwezesha mteja kuhifadhi pesa zake na kuwa na uwezo wa kutoa mara moja tu kwa mwaka, huku ukiwekeza kiasi kidogo kuanzia Sh. 10,000 kupitia ATM zetu nchi nzima," alisema Aliko Mwamusako, Meneja wa NBC Tawi la Chang'ombe.

Pamoja na ajenda ya michezo, Benki ya NBC inatoa mafunzo juu ustadi wa ajira kupitia Programu ya 'Wajibika'. Wajibika ni mkakati wa kuwafundisha vijana mbinu ambazo hawafundishwi sekondari wala chuoni, lakini ni muhimu katika kazi zao za baadaye. Mbinu hizo ni pamoja na ustadi wa kazi, stadi za fedha, ujasiriamali na stadi za kuhusiana na watu. Programu hiyo ya NBC imeshafundisha vijana zaidi ya 9000 hapa nchini.

## KVZ, Uhamiaji kazi ipo fainali FA leo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

FAINALI ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) maarufu FA Cup, kwa Upande wa Unguja inatarajiwa kupigwa leo kwa timu ya KVZ kuvaana na Uhamiaji, mchezo unaotarajiwa kupigwa katika Uwanja wa Mau A majira ya saa 10:00 alasiri.

Mshindi wa leo atakutana na mshindi wa fainali ya Kisiwani Pemba ili kuipata timu moja ambayo itaiwakilisha Zanzibar katika michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika. Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa timu ya KVZ, Khamis Abdulhamid Hamid, alisema matarajio yake makubwa ni kuona timu yake inapata nafasi ya kuiwakilisha Zanzibar katika michuano hiyo ya CAF.

Alisema wamejiandaa kuelekea mchezo huo wa fainali kwa upande wa Unguja na kwake utakuwa mgumu licha ya timu wanayocheza nayo kuwa Ligi Daraja la Kwanza.

"Timu za madaraja ya chini ni ngumu pale unapokutana nazo maana zina wachezaji wazuri, vijana na hodari na wanapokutana na timu ambayo ni ya Ligi Kuu hucheza kwa juhudi ili kuonyesha kuwa wapo vizuri, hivyo tumejiandaa kukabiliana na kila hali katika mchezo huo," alisema.

Hata hivyo, aliwataka mashabiki wa KVZ kujitokeza kwa wingi katika mchezo huo muhimu ili kuipa hamasa timu yao iweze kufanya vizuri na kutinga fainali kabla ya kukata tiketi ya kuiwakilisha Zanzibar Kombe la Shirikisho Afrika.



Ofisa Michezo wa Wilaya ya Rorya, Saidi Masanja, akimkabidhi kombe nahodha wa Town Stars, Peter Ramble, baada ya timu hiyo kutwaa ubingwa wa Umoja Cup kwa kuifunga Rifa FC mabao 3-2 kwenye fainali iliyopigwa mwishoni mwa wiki katika Uwanja wa Maji Sota, Shirati wilayani Rorya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## *Town Stars bingwa Umoja Cup 2020 Rorya*

**Na Mwandishi Wetu,** RORYA

HATIMAYE Town Stars iwetwaa ubingwa wa michuano ya Umoja Cup iliyokuwa ikitimua vumbi Uwanja wa Maji Sota, Shirati wilayani Rorya kwa kushirikisha jumla ya timu 20.

Katika mechi hiyo ya fainali iliyopigwa mwishoni mwa wiki huku ikichezeshwa kwa makini na mwamuzi Azaria Kembo, Town Stars ilibeba ubingwa huo kwa kuichapa Rifa FC mabao 3-2 kwenye mchezo huo wa fainali uliokuwa na ushindani mkali.

Town Stars ambayo ilitinga fainali baada ya kuitoa Maji FC kwa bao 1-0 kwenye nusu fainali, katika mechi ya fainali mabao yake yalifungwa na Henry na Mwinda Japhet huku la ushindi likiwekwa kambani na John Michael wakati ya Rifa FC iliyotinga hatua hiyo kwa kuichapa Bumbombi 1-0, juzi mabao yake yalifungwa na Ouma na Pawa Shemaya.

Kwa kutwaa ubingwa huo, Town Stars imejinyakulia kombe pamoja na kitita cha Sh. 300,000 huku mshindi wa pili, Rifa akiondoka na Sh. 200,000 wakati Maji FC ambayo ilipata ushindi wa bwerere kutokana na Bumbombi kutojitokeza uwanjani kwenye mechi ya kusaka mshindi wa tatu, ikikabidhiwa Sh.100, 000.

Kwa upande wa Mfungaji Bora wa Michuano hiyo, Kevin Manucho wa Town stars alikabidhiwa ngao na Sh. 15,000 sawa na Mchezaji Bora, Tumaini Atola wa Maji FC huku Kipa Bora, Doto John wa Maji FC yeye akiibuka na Sh. 15,000.

Akikabidhi zawadi na kombe kwa washindi, Mgeni Rasmi Ofisa Michezo wa Wilaya ya Rorya, Saidi Masanja, alimpongeza Mwandaaji wa Mashindano ya Umoja Cup, Peter Owino kwa kuendelea kuandaa michuano hiyo kwa kipindi cha miaka nane sasa kwa faida ya jamii nzima ya Rorya.

"Ndugu Owino tunakupongeza kwa juhudi hizi za kila mwaka, ofisi yetu ya wilaya inaahidi kukupa ushirikiano pia kukaribisha wapenda soka wengine ili kufanikisha zaidi mashindano haya kwa kuimarisha michezo mbalimbali," alisema Masanja.

Akizungumzia michuano hiyo, Owino alisema amekuwa akihamasika kuiandaa kwa kuwa mbali na kuwa burudani kwa wakazi wa Rorya, lakini lengo kubwa ni kuibua vipaji na kuikutanisha jamii pamoja ili kujenga amani na ushirikiano katika masuala mbalimbali.

"Pia mashindano haya ndiyo yanayotoa wachezaji kwenda kuunda timu ya Maji inayoshiriki Ligi ya Mkoa," alisema Owino.

Michezo
Jumanne Agosti 18, 2020
Nipashe



Aubameyang akubali kusaini mkataba UKURASA 22

IMEISHA HIYO...




Kiungo wa Sevilla, Muargentina Ever Banega, akiwania kumiliki mpira dhidi ya kiungo wa Manchester United, Mfaransa Paul Pogba, kwenye mechi ya nusu fainali ya Ligi ya Europa iliyopigwa juzi usiku katika Uwanja wa RheinEnergie jijini Cologne, Ujerumani. Sevilla ilishinda 2-1 na huo ukawa mwisho wa United msimu huu. **HABARI UK. 21**

## Yanga yaanza na Tonombe, Kisinda

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI watani zao wa jadi, Simba, wakitangaza kufunga rasmi mchakato wa usajili juzi, kikao kizito kimefanyika jana nchini DR Congo kati ya uongozi wa Klabu ya AS Vita na Yanga zikitaka kukamilisha biashara kwa viungo wao, Mukoko Tonombe na Tuisila Kisinda.

Tajiri wa Yanga, Mkurugenzi wa Uwekezaji wa GSM, Injinia Hersi Said, ambaye wanaidhamini kupitia kampuni hiyo, jana alifanya mkutano mzito AS Vita kwa ajili ya kuwanunua wachezaji wa klabu hiyo.

Licha Hersi kutowataja, lakini Nipashe linafahamu kuwa wachezaji Yanga inaowataka ni winga, Kisinda na kiungo mkabaji Tonombe.

"Nimepokelewa vizuri hapa AS Vita, na leo (jana) tunakutana kufanya mazungumzo, kuna wachezaji tunawahitaji hapa wapo timu ya taifa wanacheza michuano ya ndani, sisi sio chama cha kuleta wazee ambao wameshazunguka huku na huko.

"Mambo yetu tunayapeleka kwa taratibu, hatuwezi kuwa kama wengine ambao wanavizia wakisikia kuna mchezaji tunamtaka basi wanakimbilia kumsajili," alisema Hersi.

Kuhusu uwezekano wa kuipata huduma ya Kocha Mkuu wa As Vita, Florent Ibenge, Injinia Hersi alisema: "Hapana uongozi wao umeniambia hauwezi kumwachia kwa sasa."

# SIMBA, YANGA NANI ZAIDI SASA OKTOBA 18

## ●●● Majibu kwa Mkapa, Matola asema wamekamilika, Wanajangwani wakisema subirini...

**Na Saada Akida**

KIPENGA cha Ligi Kuu Bara kimepulizwa rasmi baada ya Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), kutangaza rasmi ratiba ya michuano hiyo itakayofunguliwa Septemba 6, mwaka huu kabla ya kukaribishwa na mechi ya Ngao ya Jamii kati ya Simba na Namungo itakayopigwa Agosti 29 katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

**Hata hivyo, baada ya kila timu kuwa 'bize' katika dirisha la usajili hususan watani wa jadi, Simba na Yanga, TPLB imetangaza miamba hiyo itakutana Oktoba 18, mwaka huu katika mechi ya raundi ya kwanza ambayo Wanajangwani hao watakuwa wenyeji kwenye mchezo huo utakaopigwa Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam.**

Mchezo huo wa watani wa jadi unatarajiwa kujibu maswali ya nani kasajili vizuri zaidi msimu huu, lakini pia Yanga ikitaka kulipa kisasi cha kufungwa mabao 4-1 kwenye mechi ya mzunguko wa pili msimu wa 2019/20.

Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almas Kasongo, akitangaza ratiba hiyo jijini Dar es Salaam jana, alisema baada ya mechi ya Oktoba 18, watani hao wa jadi watarudiana Februari 20, mwakani katika mchezo wa mzunguko wa pili utakaopigwa uwanjani hapo.

Kwa upande wa mechi za ufunguzi, Simba itaanzia jijini Mbeya Septemba 6 dhidi ya timu iliyopanda Ligi Kuu msimu huu, Ihefu FC wakati Yanga ikiwa Uwanja wa Mkapa kuikaribisha Tanzania Prisons ya Mbeya.

Siku hiyo hiyo, Namungo FC itakuwa mwenyeji wa Coastal Union katika Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi, wakati Biashara United ikialika timu nyingine iliyopanda daraja msimu huu, Gwambina FC ya Mwanza huku Mtibwa Sugar ikiikaribisha Ruvu Shooting.

Raundi ya kwanza itakamilika Septemba 7, kwa KMC FC kuikaribisha Mbeya City huku Kagera Sugar ikiwa mwenyeji wa JKT Tanzania wakati Azam FC ikiialika Polisi Tanzania.

Aidha, Kasongo alisema ligi hiyo ambayo itashirikisha timu 18 kutoka 20 za msimu uliopita, itamalizika Mei 15, mwakani kwa kuchezwa jumla ya mechi 306 badala ya 380 za msimu wa 2019/20.

"Tumepanga ratiba kuzingatia Kalenda ya Shirikisho la Soka duniani (FIFA) na CAF kabla ya wao kutoa yao, tumekisia kwa kalenda za matukio yao na kama kutakuwa na mabadiliko nina imani yatafanyiwa kazi kwa kubadili," alisema Kasongo.

Alisema katika ratiba hiyo kumekuwa na uwiano mzuri wa mechi kwa kucheza mechi 17 za nyumbani na 17 ugenini, kwa timu kucheza kati ya mechi saba au nane nyumbani.

"Mechi kubwa ya Simba dhidi ya Yanga itachezwa Oktoba 18, mwaka huu itakuwa siku ya Jumapili Uwanja wa Mkapa, Saa 11:00 jioni," alisema Kasongo.

Baada ya ratiba hiyo kutoka, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Fredrick Mwakalebela, aliliambia Nipashe kuwa kwa upande wao wana imani na Bodi ya Ligi kwa kupanga ratiba ambayo haijambeba au kupendelea timu yoyote.

"Kuhusu pambano letu dhidi ya Simba ni mechi ambayo haikwepeki, kikubwa tumejipanga vizuri kuhakikisha msimu huu tunafanya vizuri kwa kulipa kisasi kwa mtani wetu kwani mechi ya mwisho alitufunga mabao 4-1," alisema Mwakalebela huku akiamini katika usajili walioufanya kuwa utawawezesha kufikia malengo yao.

Kuhusu kocha, alisema: "Mchakato unaendelea na tupo sehemu nzuri ya kupitia maombi ya CV zilizotumwa na ndani ya wiki hii atajulikana na kutangazwa."

Kwa upande wa Simba, ambayo jana ilingia kambini rasmi, awali kabla ya ratiba hiyo kutoka, Kocha Msaidizi, Selemani Matola, alisema benchi la ufundi limetimiziwa mahitaji yao ya usajili kwa asilimia 100.

"Usajili umekamilika, na nafasi tulizopendekeza kuongezewa nguvu uongozi umefanya hivyo na si tu kusajili bali kusajili wachezaji tuliowahitaji, unajua unaweza kupendekeza majina mengi na kati yao akapatikana mmoja wao," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >